SportPesa
CHEZA USHINDE SASA
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

UKURASA 2

ACT WAZALENDO

**ACT-Wazalendo yazindua kampeni ikimnasa kiongozi wa vijana CUF**

**HARUSI**



UKURASA 12

Jumapili Februari 6, 2022 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe JUMAPILI

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com

ISSN 0856 • No. 0580848

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

**RIPOTI MAALUM**

# Kilichojificha mauaji yanayotikisa nchini

**Mwalimu** auawa kikatili, wanasaikolojia, viongozi wa dini wanena... *Endelea ukurasa 2 & 4*




Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Rais Samia Suluhu Hassan, akipokea mfano wa kadi yake namba moja ya kielektroniki ya uanachama wa CCM, kutoka kwa Katibu Mkuu wa chama hicho, Daniel Chongolo, baada ya kuzindua rasmi zoezi la ugawaji wa kadi hizo, katika kilele cha maadhimisho ya Miaka 45 ya kuzaliwa chama hicho, katika Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara jana. Kulia ni Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi. **PICHA: IKULU**

# Samia amulika walioanza kampeni mapema CCM

UKURASA 2

## Kiti cha Naibu Spika chavuta vigogo CCM

UKURASA 2

MICHEZO SIMBA YAIWINDA MBEYA KWANZA UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

# Mwalimu auawa kikatili

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MWALIMU wa Shule ya Msingi Kisokwe Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Albert Kaguli (43), amekutwa ameuawa na watu wasiojulikana huku chanzo cha mauaji kikidaiwa kuwa wivu wa mapenzi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga alithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana wilayani humo, akisema mwalimu huyo aliuawa kwa kupigwa na kitu kizito kichwani huku Jeshi hilo likimtafuta Shukuran Maselo kwa tuhuma za mauaji hayo.

"Chanzo cha tukio hili inasadikiwa kuwa ni wivu wa mapenzi dhidi ya mtuhumiwa wa kosa hili, bado Jeshi la Polisi linaendelea na uchunguzi ili kubaini watuhumiwa wengine wa mauaji hayo ya kikatili," alisema.

Alibainisha kuwa tukio hilo ni la tano kutokea mkoani humo mwaka huu na jeshi linaendelea kuwasaka wahalifu hao ili kuwachukulia hatua za kisheria.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Josephat Maganga, alilaani mauaji hayo na kuwataka wananchi kuacha kujichukulia sheria mkononi.

# ACT yazindua kampeni ikimnasa kiongozi wa CUF

**Na Romana Mallya**

CHAMA cha ACT-Wazalendo kimezindua operesheni ya 'Shusha Tanga Pandisha Tanga' awamu ya pili huku kikimpokea Hamidu Bobali, aliyekuwa Mwenyekiti wa Jumuiya ya Vijana ya Chama cha Wananchi (CUF) na Mbunge wa Mchinga.

Machi 18, 2019, aliyekuwa Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo, Maalim Seif Shariff Hamad, alitangaza operesheni hii akiwataka wanaomuunga mkono katika mapambano ya kupigania haki kujiunga na ACT-Wazalendo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shaibu, Bobali alishasajiliwa jana kwenye programu ya ACT-Kiganjani na kupata kadi ya uanachama.

Shaibu alisema kuwa mwaka 2019 baada ya operesheni hiyo kuzinduliwa, maelfu walijiunga na chama hicho.

"Katika kipindi cha wiki moja kuanzia Machi 19, 2019, zaidi ya wanachama 100,000 walijiunga na ACT-Wazalendo na kubadili kabisa ramani ya kisiasa nchini," alisema.

Shaibu alisema kuwa mwaka mmoja baada ya Uchaguzi Mkuu wa 2020, wapo viongozi waandamizi wa vyama mbalimbali wamekuwa wakiomba kujiunga na chama chao.

# Rais Samia aonya walioanza kampeni

**Na Waandishi Wetu,** MUSOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimetangaza utaratibu mpya wa kuadhimisha sherehe za kuzaliwa kwake kitaifa wa kila baada ya miaka mitano, huku Mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan akitoa onyo kwa wanachama walioanza kampeni mapema.

Rais Samia alitoa onyo hilo jana mjini Musoma mkoani Mara wakati wa kilele cha maadhimisho ya miaka 45 tangu kuzaliwa kwa chama hicho, akisema sherehe hizo kwa kila mwaka zitakuwa zinaadhimishwa kimkoa.

Alisema uchaguzi ndani ya chama utafanyika mwaka huu na kubainisha kuna watu wameanza harakati za kutaka uongozi mkoani Mara kabla ya muda.

Alisema jicho la chama lipo wazi kwa wanaoanza kampeni kabla ya muda.

Rais Samia alisema chama hicho kilifanya matembezi ya hisani na kukusanya Sh. milioni 300 ambazo ameelekeza zitumike kutengeneza kadi za kielektroniki.

Kiongozi huyo pia alibainisha mafanikio katika sekta mbalimbali zikiwamo kilimo na kupongeza Tanzania kufikia uchumi wa kati kabla ya mwaka 2025.

Sherehe hizo zilifanyika kwa mara ya pili mkoani Mara tangu kuzaliwa CCM, zilihudhuriwa na makatibu wakuu wastaafu wa chama hicho na viongozi wengine wa kitaifa wakiamo Rais mstaafu, Jakaya Kikwete, Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, Waziri Mkuu, Kasim Majaliwa pamoja na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Akson.

■ **Imeandikwa na Richard Makore na Beatrice Shayo**



Makamu wa Rais, Dk. Philip Isdor Mpango akishiriki katika ufunguzi wa Mkutano wa 35 wa Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika (AU), jijini Addis Ababa, Ethiopia jana. Mkutano huo, umebeba kauli mbiu isemayo "Kuimarisha Lishe na Usalama wa Chakula barani Afrika: Kuongeza kasi ya Uzalishaji katika Kilimo, Maendeleo ya Rasilimali Watu na Maendeleo Endelevu ya Kiuchumi na Kijamii". **PICHA: OMR**

# Kiti cha Naibu Spika chavuta vigogo CCM

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WABUNGE saba wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wamejitokeza jana kuchukua fomu za kuomba ridhaa ya kuteuliwa na chama kugombea nafasi ya Naibu Spika wa Bunge.

Kati ya wabunge hao waliojitokeza jana, yumo Mbunge wa Ilala, Mussa Azan Zungu, Mbunge wa Nzega Vijijini, Dk. Hamis Kigwangalla, pamoja na mdogo wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mbunge wa Mahonda Mkoa wa Kaskazini Ugunja, Abdullah Ali Mwinyi.

Wengine ni Mbunge wa Hanang, Samweli Xaday, Mbunge wa Mwanga Joseph Anania, David Kihenzele wa Mufindi Kusini na Dk. Oscar Kikoyo wa Muleba Kusini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana mara baada ya kuchukua fomu, Mbunge wa Mahonda, Abdullah Ali Mwinyi, alisema ana imani anaweza kuitumikia nafasi ya Unaibu Spika iwapo chama chake kitampitisha kugombea nafasi hiyo.

"Nina uzoefu wa kutosha katika nafasi hii ya ubunge na nimeongoza wabunge katika Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambalo kimsingi halina utofauti na uendeshaji wa Bunge hili, tofauti labda ni lugha tu kule ni Kiingereza na hili ni Kiswahili, hivyo ninaamini naweza kuongoza kama nitapewa ridhaa na chama changu," alisema.

Aliongeza kuwa anao uzoefu wa kuwa mbunge kwa vipindi vitatu tofauti ambapo mara mbili amekuwa Mbunge wa Bunge la Afrika Mashariki na sasa ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

"Mimi ni mwanasheria mzoefu, ninaimani nina uwezo wa kuitumikia nafasi ya Unaibu Spika kwa kutumia utulivu, hekima pamoja na maarifa," alitamba.

Dk. Kigwangalla alisema sababu iliyomsukuma kuchukua fomu ya kuwania kiti hicho ni sifa alizonazo kwa mujibu wa katiba ya nchi.

"Ninazo sifa kwa mujibu wa katiba ya nchi na chama changu lakini pia kanuni za uchaguzi ndani ya chama zinaniruhusu ndani ya chama na tume lakini pia ninao uzoefu wa kutosha kuongoza wabunge wenzangu na nimewahi kushika nafasi serikalini kama vile uwaziri na unaibu waziri," alisema Dk. Kigwangwala.

Zungu alisema amechukua fomu ya kuwania kiti hicho kutokana na kuwa wazi.

Uchukuaji na urudishaji wa fomu za kuomba uteuzi wa kuwania nafasi hiyo unatarajiwa kufungwa leo saa 10:00 jioni.

HABARI KITAIFA

## MUHAS yapewa milioni 100/- kukabili UVIKO-19

**Na Faustine Feliciane**

FAMILIA ya aliyekuwa Waziri Mkuu wa Tanzania, Salim Ahmed Salim, kupitia Mfuko wa Amne Salim, imetoa Sh. milioni 100 kwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya Muhimbili (MUHAS) kufadhili utafiti wa ndani juu ya ugonjwa wa UVIKO-19.

Fedha hizo zimetolewa ikiwa ni sehemu ya kumbukumbu ya kifo cha mke wa Dk. Salim, Amne Salim, aliyefariki dunia kwa ugonjwa huo Oktoba mwaka 2020.

Akizungumza wakati wa kuwatangaza washindi wa mchakato wa kuwapata wataalamu wa afya watakaofanya utafiti huo, Makamu Mkuu wa MUHAS, Profesa Andrea Pembe, alisema utafiti unaokwenda kufanywa na washindi wanane waliopatikana kati ya wataalamu 24 waliowasilisha dokezo, unalenga mabadiliko ya kitabia ya virusi hivyo, historia ya ugonjwa pamoja na namna ya kukabiliana nao.

"Mchakato wa kuwapata wataalamu hawa walioshinda ulikuwa wa wazi na kuendeshwa na kamati maalumu baada ya mazungumzo na familia ya Amne Salim.

"Matokeo ya utafiti huo yatalisaidia taifa katika kukabiliana na mabadiliko ya ugonjwa huo wa UVIKO-19," alisema Profesa Pembe.

Alisema mchakato wa kuwapata washindi ulianza Oktoba mwaka jana na matokeo ya utafiti utakaofanywa yanatarajia kukamilika Oktoba mwaka huu wakati wa maadhimisho ya kifo cha Amne Salim.

Profesa Pembe alisema kuwa kati ya fedha hizo Sh. milioni 100 zilizotolewa, Sh. milioni 97 zitagawanywa kwa washindi hao wanane kulingana na andiko la kila mmoja.

Akizungumza kwa niaba ya familia, mtoto wa Dk. Salim, Ahmed Salim, alisema kuwa kama familia wamefarijika kuona wataalamu wa ndani wanakwenda kufanya utafiti utakaokisaidia chuo kikuu hicho na taifa kwa ujumla.

"Wazo la kuanzishwa programu tulilipata mara baada ya mama yangu (Amne Salim) kufariki dunia Oktoba mwaka 2020, mama alikuwa mtu wa kuchangia sana kwa jamii hususani kwenye mipango ya kimaendeleo kwa taifa na jamii.

"Katika kumuenzi ndipo tukaja na wazo hili, kwa kushirikiana na marafiki tumekusanya na kukabidhi fedha hizi ili ziweze kusaidia taifa kwenye mapambano dhidi ya corona," alisema Ahmed.

Alisema marafiki zao Taasisi ya The Karimjee Jivanjee Foundation wameongeza dola 5,000 (zaidi ya Sh. milioni 12) ambazo wamezikabidhi kwa MUHAS.

"Amne Fund tutaendelea kuchangia kwa jamii hata kwa masuala mengine baada ya hili la utafiti wa Covid-19," alisema Ahmed.

Walioshinda kupatiwa fedha hizo ni wataalamu wa masuala ya afya kutoka MUHAS ambao ni Lilian Nkinda, Profesa Karim Manji, Zainab Hassan Yusuph, Dk. Obrey Harold, Alphoncina Kagaigai, Dk. Mourice Mbunde, Godwin Pancras na Leonida Kanyuma.

Mmoja wa wataalamu hao, Godwin Pancras, ambaye anakwenda kufanya utafiti wake mkoani Geita, alisema utafiti wanaofanya utakisaidia chuo na taifa kwa ujumla katika kuufahamu zaidi ugonjwa wa UVIKO-19 na namna ya kukabiliana nao kitaifa.

Alisema watajitahidi kukamilisna utafiti huo katika kipindi kilichopangwa na kuwasilisha chuoni huko.



Mkuu wa Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Halima Bulembo akiandika namba moja kwenye moja ya nyumba, katika barabara ya Mtaa wa Akida, Kata ya Masuguru, wakati akizindua mfumo wa anuani za makazi, wilayani humo jana. Kushoto kwake ni Mwenyekiti wa Kamati ya Anuani za Makazi Wilaya, Thomas Mkwavi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Madarasa yageuzwa kituo cha kuvuta bangi

**Na Moshi Lusonzo**

WANAFUNZI wanaosoma katika shule mbili za msingi za Kijichi wilayani Temeke mkoani Dar es Salaam, wako hatarini kuathirika kiafya na kimaadili kutokana na madarasa yao kutumika kama sehemu ya kuvuta bangi.

Vitendo hivyo vimefichuliwa juzi na viongozi wa Jumuiya ya Wazazi Kata ya Kijichi waliotembelea shule hizo kwa ajili ya kutoa misaada kwa wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu katika kuadhimiashia miaka 45 ya kuzaliwa Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Akizungumzia suala hilo, Mwalimu Mkuu Msaidizi wa Shule ya Msingi Kijichi B, Stephano Cherehani, alisema matumizi ya dawa hizo za kulevya tayari yameonekana kuwa na athari katika maendeleo ya elimu kutokana na baadhi ya wanafunzi kupata madhara.

Alisema watu wanaoingia shuleni huko kila siku kwa nia ya kuangalia michezo ya mpira wa miguu, hutumia madarasa kuvuta bangi na kuacha mabaki kila mahali.

Cherehani alisema wakati mwingine watu hao wanavuta nje ya madarasa hayo kipindi cha asubuhi, jambo ambalo linaleta usumbufu kwa wanafunzi wanapotaka kuingia darasani kuanza vipindi vya masomo.

"Jambo hili linatuathiri sisi walimu na wanafunzi pia, uvutaji wa bangi umekuwa kama jambo la kawaida, lakini chanzo kikubwa ni huu uwanja wa mpira ambao unatumika na jamii muda wote," alisema.

Aliomba serikali kuingilia kati kwa kudhibiti vitendo hivyo ili kuwaweka wanafunzi katika hali ya utulivu na kukidhi matakwa ya mazingira bora ya ujifunzaji na ufundishaji.

"Wanafunzi hawawezi kusoma kwa umakini kama kuna mabaki ya bangi au mtu anavuta nje ya darasa, tunaomba watu hawa wadhibitiwe haraka," alisema.

Katibu wa Wazazi wa CCM katika kata hiyo, Magdalena Komba, alimhakikishia mwalimu mkuu huyo kuwa watalifanyia kazi haraka kwa kwenda kuripoti katika vyombo husika ili eneo hilo liwe salama kwa utoaji wa elimu kwa watoto.

"Pamoja na kwamba leo (juzi) tumekuja kuwasaidia watoto wetu wanaoishi katika mazingira magumu, lakini suala hili la uvutaji bangi holela limenigusa na nitakwenda kuwasiliana na vyombo husika ili kulikomesha," aliahidi.

Komba pia alisema jumuiya hiyo ni sawa na kiranja katika malezi ya watoto na ndio maana katika maadhimisho hayo, wameamua kutoa misaada ya sare za shule na madaftari kwa wanafunzi 27 wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Mwanafunzi Hamisi Shamte aliyenufaika na msaada huo, aliishukuru jumuiya hiyo kwa kuwatambua na kisha kuwapa msaada huo ambao utawasaidia katika safari yao ya elimu.

Diwani wa Kijichi, Athuman Nyamlani, aliahidi kuliwasilisha suala hilo kwenye vyombo vya dola ili wanaojihusisha na vitendo hivyo wachukuliwe hatua za kisheria.

# Msako wanafunzi 700 watangazwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** KARATU

UONGOZI wa Wilaya ya Karatu mkoani Arusha umetangaza kuanza operesheni ya kata kwa kata na nyumba kwa nyumba kuwasaka wanafunzi 699 ambao ni kati ya 4,000 waliochaguliwa kujiunga na sekondari mwaka huu lakini hadi sasa hawajaripoti shuleni.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Dadi Kolimba, alitangaza jana operesheni hiyo itakayoanza kesho alipokuwa kwenye maadhimisho ya miaka 45 ya kuzaliwa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) ambayo kimkoa yalifanyika mjini Karatu.

Kolimba alisema Wilaya ya Karatu ilipokea Sh. bilioni 1.2 ambazo zimetumika kujenga madarasa 60 ambayo yamekamilika lakini mpaka sasa wanafunzi 3,301, sawa na asilimia 74 kati ya 4,000 waliochaguliwa kuendelea na sekondari ndio walioripoti shuleni.

"Nitumie hadhara hii kuwaeleza wazazi ambao watoto wao hawajajiunga shuleni, wiki ijayo tunaanza kampeni ya kata kwa kata, nyumba kwa nyumba ili kuhakikisha vijana wote waliochaguliwa wanajiunga na sekondari, haiwezekani serikali itoe fedha halafu vijana wasijiunge na shule," alionya.

Aliongeza kuwa katika sekta ya elimu wilaya hiyo pia ilipokea Sh. milioni 700 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa Shule ya Sekondari Karatu na kazi imefanyika vizuri.

Kuhusu sekta ya afya, alisema Wilaya ya Karatu ilipokea Sh. bilioni mbili kwa ya ujenzi wa jengo la utawala, OPD (jengo la wagonjwa wa nje), maabara na chumba cha dawa ambapo ujenzi wake unaendelea vizuri.

Kolimba alisema wilaya pia ilipokea Sh. bilioni 2.75 za tozo ya miamala ya simu ambazo zimepelekwa kujenga kituo cha afya Buga Nyekundu na kwamba kimsingi utekelezaji wa ilani katika wilaya hiyo unakwenda kwa kasi anayoihitaji.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Karatu, John Lucian, alisema serikali imeendelea kutoa fedha kwa Wilaya ya Karatu kwa ajili ya ujenzi wa miradi mbalimbali ya maendeleo.

"Kazi kubwa inafanyika katika wilaya yetu, madarasa yanajengwa kila mahali, miradi ya afya na hata ujenzi wa barabara unafanyika hadi zile ambazo toka Yesu Kristo azaliwe hawajawahi kuona greda. Kwa niaba ya wananchi wa Karatu tunamshukru Rais Samia Suluhu Hassani," alisifu.

Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Arusha, Zelothe Stephen, alisema madarasa 513 ya fedha za UVIKO yamejengwa na kukamilika katika mkoa huo.

RIPOTI MAALUMU

# Kilichojificha mauaji yanayotikisa nchini

## ■Mapenzi, tamaa ya mali sehemu ya tatizo
## ■Rais Samia, Majaliwa wachukua hatua
## ■Wanasaikolojia, viongozi wa dini wanena



Rais Samia



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa



Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga

**Na Waandishi Wetu**

KATIBA ya Tanzania ya Mwaka 1977 katika sehemu yake ya utangulizi inajipambanua kwamba Watanzania wameamua rasmi na kwa dhati kujenga katika nchi yao jamii inayozingatia misingi ya uhuru, haki, udugu na amani.

Ibara ya 14 ya Katiba hiyo inatamka: "Kila mtu anayo haki ya kuishi na kupata kutoka kwa jamii hifadhi ya maisha yake, kwa mujibu wa sheria."

Vilevile, kwenye Ibara ya 15 ya Katiba hiyo inatamka: "Kila mtu anayo haki ya kuwa huru na kuishi kama mtu huru. Kwa madhumuni ya kuhifadhi haki ya mtu kuwa huru na kuishi kwa uhuru, itakuwa ni marufuku kwa mtu yeyote kukamatwa, kufungwa, kufungiwa, kuwekwa kizuizini, kuhamishwa kwa nguvu au kunyang'anywa uhuru wake vinginevyo, isipokuwa tu katika hali na kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sheria, au katika kutekeleza hukumu, amri au adhabu iliyotolewa na mahakama kutokana na shauri au na mtu kutiwa hatiani kwa kosa la jinai."

Hata hivyo, kinachoshuhudiwa sasa ni ukiukwaji wa misingi hiyo iliyowekwa na Katiba, kukishuhudiwa idadi kubwa ya matukio ya mauaji ya watu kwenye maeneo mbalimbali nchini.

Hatua zilizochukuliwa na serikali hadi sasa kukabiliana na baa hilo ni pamoja na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Masauni, kukutana na viongozi waandamizi wa Jeshi la Polisi, wizara kuunda kamati ya kuchunguza matukio ya mauaji nchini na juzi Rais Samia Suluhu Hassan alimwagiza Waziri Mkuu kuunda tume ya kuchunguza mauaji yaliyofanywa na Jeshi la Polisi mkoani Lindi.

Katika kutekeleza agizo hilo la Rais, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, aliunda kamati maalumu yenye wajumbe tisa kuchunguza mauaji yaliyofanywa na Jeshi la Polisi mkoani Mtwara na mauaji ya watu sita yaliyotokea Januari 30 huko Kilindi mkoani Tanga.

**MATUKIO 20 JANUARI**

Ripoti ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), iliyotolewa wiki iliyopita, ilibainisha kuwapo matukio 20 ya mauaji yaliyoripotiwa nchini katika kipindi cha siku 27 za mwanzo wa mwaka huu.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, akizungumza na waandishi wa habari mkoani Dar es Salaam Januari 27 mwaka huu, alisema katika kipindi hicho matukio hayo yaliripotiwa na kusababisha ukiukwaji wa haki za binadamu.

Kutokana na matukio hayo kukithiri, alisema LHRC inatoa wito kwa wanasaikolojia, watetezi wa haki za binadamu na viongozi wa kijamii kutumia muda wao kuelimisha umma.

"Kituo cha sheria kimekusanya takribani matukio 20 ya mauaji hayo yaliyoripotiwa katika mikoa ya Mtwara, Rukwa, Njombe, Katavi, Mwanza, Dodoma, Ruvuma, Dar es Salaam na Mara,"alibainisha Anna.

Ripoti ya LHRC ya mwaka 2020 ilibainisha kuendelea kushamiri kwa vitendo mbalimbali vya ukiukwaji wa haki ya kuishi, ikiwamo matukio 32 ya wanawake kuuawa na wenza wao. Kati yake, matukio 23 yalihusishwa na wivu wa kimapenzi.

**KIINI CHA TATIZO**

Mchungaji Dani Sendolo wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Mashariki na Pwani, anazitaja baadhi ya sababu zinazochangia mauaji hayo kuwa ni pamoja na wivu wa mapenzi, imani potofu za kishirikina, migogoro ya ardhi, tamaa ya mali, migogoro ya kimila pamoja na tatizo la afya ya akili.

Mchungaji Sendolo ambaye pia ni mtaalamu wa saikolojia na mratibu wa makundi maalumu wa KKKT katika dayosisi hiyo, anawashauri wazazi kuwapenda watoto wao pasi na kuwaonyesha ubaguzi, akifafanua kuwa wanapaswa kuepuka kuegemea upande mmoja.

Mwanasaikolojia huyo pia anashauri wazazi na walezi kuacha kuwajaza alichokiita 'sumu kupita kiasi' (maneno yenye kutia uchungu) watoto wao pamoja na jamii kutenda haki katika utatuzi wa migogoro yao.

"Jamii inapaswa kutowanyanyapaa wenye ulemavu wa akili, iwasaidie kutatua kero zao kwa upendo, hili litapunguza mauaji yasiyokuwa ya lazima," anashauri Mchungaji Sendolo.

Mchungaji mstaafu wa KKKT na mbobezi katika utatuzi wa migogoro, Christosila Kalata, anasema hakuna njia mbadala ya kutokomeza vitendo vya mauaji nchini, zaidi ya jamii kurejesha upendo wa awali.

Anasema kukosekana kwa upendo wa mtu na mtu, jamii na jamii ni sababu kubwa ya kuchochea vitendo vya ukatili wa kutisha yakiwamo mauaji ya watu yanayotikisa nchini kwa sasa.

Kiongozi huyo wa kiroho anasema jamii ina jukumu kubwa la kutokomeza mauaji yanayoendelea nchini kwa kuhakikisha kila mtu atajiona ni sehemu ya mkakati huo.

"Jamii ijifunze kuhurumiana na kutafuta suluhu ya migogoro mapema kwa njia ya haki badala ya kungoja mpaka majanga yanapotokea," anasema.

Mchungaji Kalata ambaye pia ni mjumbe wa Kamati ya Amani Mkoa wa Dar es Salaam, anafafanua kuwa kukosekana kwa haki, upendo na ushirikiano kati ya wazazi, ndugu, jamaa na marafiki, kumesababisha "kila mtu kutazama maslahi yake binafsi kuliko maagizo ya Mwenyezi Mungu ambaye ameasa kumpenda jirani kama nafsi zetu".

Anabainisha: "Sababu kubwa ya mauaji ya kikatili kutokea ni kutafuta furaha ya nafsi kutokana na uchungu alionao mtu, aidha kwa kusimuliwa mambo mabaya yaliyotokea awali au kuyashuhudia mwenyewe."

**■Imeandikwa na Daniel Limbe (GEITA) na Ayubu Mpanja**

## SIDO kuwezeshwa kuendeleza viwanda

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imesema itaendelea kuliwezesha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) ili kuboresha mfumo wa uendeshaji na utoaji wa huduma bora na wezeshi zinazotumia teknolojia ya kisasa.

Hatua hiyo inalenga kuliwezesha shirika hilo kuongeza ajira na kukuza uchumi wa nchi.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Prof. Godius Kahyarara, aliyasema hayo juzi wakati akitoa taarifa ya utendaji ya shirika hilo kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) kuhusu utekelezaji wa majukumu na mafanikio yake, katika ukumbi wa Bunge jijini Dodoma.


Kutokana na umuhimu wa SIDO nchini, kamati hiyo imeliagiza shirika hilo kuongeza juhudi katika kuwezesha Watanzania kuanzisha viwanda vidogo vya kuzalisha bidhaa muhimu kwa kutumia teknolojia ya kisasa na mahitaji ya soko ili kupunguza utegemezi na uagizaji wa bidhaa hizo nje ya nchi, pia kuongeza ajira na pato la taifa.

Awali, akitoa taarifa ya utendaji, Mkurugenzi wa SIDO, Mhandisi Prof. Sylvester Mpanduji, alisema shirika limeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kutoa huduma za kiufundi na maendeleo ya teknolojia.

Majukumu mengine ni uanzishaji wa miradi ya viwanda vidogo vijijini, mafunzo, ushauri na huduma za ugani, masoko na habari pamoja na huduma za fedha kwa wajasiriamali wadogo.

Alisema SIDO imeendelea kujenga mabanda (industrial shades) katika kila mkoa yanayowawezesha wajasiliamali kuanzisha viwanda katika maeneo hayo kwa urahisi na hadi sasa shirika lina mitaa ya viwanda katika mikoa 21 ambayo ina majengo ya viwanda 673 yanayotumiwa na viwanda 573 yenye ajira 5,297.

Pia alisema SIDO imejipanga kutanua uwigo wa utuoaji huduma inayopatikana katika mikoa yote na kuelekeza huduma hizo katika kila wilaya ili kuongeza kasi ya uanzishaji na ukuzaji wa viwanda vidogo nchini ambavyo vitaongeza ajira na kukuza biashara na uchumi wa nchi.



Rais wa Rotary Klabu ya Dar es Salaam Mzizima, Dk. Hawa Mkwela (kulia), akikabidhi sehemu ya vitabu vya uongozi kwa Mlezi wa Klabu hiyo katika Shule ya wasichana ya Jangwani, Mwalimu Ayoub Msuya na Rotarakta Joan Chundu, shuleni hapo, jijini humo, mwishoni mwa wiki. Klabu hiyo, pia ilitoa mafunzo ya uongozi kwa wanafunzi sanjari na hafla ya kukabidhi msaada wa vitabu 300 kwa vijana ambao hawajawa wanachama kamili wa klabu (Intaraktazi). Kushoto ni mtunzi wa kitabu hicho, Lion Ntandeki Nshala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Auawa kwa tuhuma kutaka kuiba pikipiki

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

YUSUPH Mgenda (24), mkazi wa Mtaa wa Msamvu A, Manispa ya Morogoro, ameuawa kwa kupigwa na wananchi wenye hasira kisha mwili wake kuchomwa moto baada ya kutuhumiwa kutaka kupora pikipiki katika Kijiji cha Pangawe, Kata ya Mkambalani wilayani Morogoro.

Akizungumza na Nipashe jana, Mwenyekiti wa Kijiji cha Pangawe, Rajabu Sudi, alisema tukio hilo limetokea jana majira ya saa nne asubuhi, akidai kuwa akiwa nyumbani kwake, alishuhudia kundi kubwa la madereva wa pikipiki (bodaboda) wakielekea shambani lilikotokea tukio hilo.

Alisema alilazimika kufika sehemu ya tukio na kukuta mauaji hayo yameshafanyika, baadhi ya mashuhuda wakidai kuwa kijana aliyeuawa alikuwa amekodisha pikipiki akiwa na mwenzake wakitokea Kata ya Bigwa na baada ya kufika katika eneo hilo, wakaanza purukushani ya kutaka kupora bodaboda hiyo. “Kwa mujibu wa shahidi hapa alisema yeye aliwakuta watu wawili wakizozana na dereva wa bodaboba.

Waliposimama kutaka kujua nini kinaendelea, ndipo dereva huyo alieleza kuwa watu hao wanataka kumwibia pikipiki na baadaye watu hao wakaanza kukimbilia mashambani na mmoja wao alikamatwa na wakulima waliokuwa karibu,” alisema.

Aliongeza kuwa vitendo hivvo vimekuwa vikijitokeza mara kwa mara katika kijiji chake ambapo baadhi ya waharifu hasa wa wizi wa pikipiki, hufanya matukio katika maeneo mengine na kukimbilia kwenye kijiji hicho chenye sifa ya kuwa na mapori.

Majuto Masharubu, shuhuda mwingine wa tukio hilo, alisema baada ya kuwakuta watu hao wakimshambulia dereva mwenzake wa bodaboda, alilazimika kuingilia kati na kufanikiwa kuwazidi nguvu ambapo wezi hao baada ya kuzidiwa, walikimbilia shambani.

Alisema baada ya watu hao kuanza kukimbia walipiga kelele za kuomba msaada ndipo wakulima waliokuwa mashambani jirani na tukio hilo walijitokeza na kuwakimbiza huku yeye akibakia eneo la tukio akilinda pikipiki zao pamoja na kufanya mawasiliano ya kuomba msaada kwa madereva waliopo maeneo ya jirani.

Ibrahim Nassoro ni ndugu wa marehemu, alidai kuwa aliyeuawa ni shemeji yake na alikuwa maarufu kwa jina la Ngeja na walikuwa wakiishi wote Mtaa wa Msamvu Shule, Manispaa ya Morogoro

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, Fortunatus Musilimu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo jana majira ya saa nne asubuhi na kwamba mwili wa marehemu ulikuwa umeshafanyiwa uchunguzi na ulitarajiwa kukabidhiwa kwa ndugu kwa ajili ya mazishi.

## Serikali yaunda tume kuwachunguza polisi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ameunda timu maalumu ya watu tisa ambayo imepewa jukumu la kuchunguza mauaji yaliyofanyika Mtwara na Kilindi mkoani Tanga.

“Kamati hiyo inapaswa kuanza kazi yake kesho (jana) na inatakiwa iwe imekamilisha ripoti yake ndani ya siku 14,” Majaliwa alisema juzi jioni ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Rais Samia Suluhu Hassan alilolitoa juzi asubuhi mjini Magu mkoani Mwanza akiwa njiani kuelekea Musoma, Mara kwenye maadhimisho ya miaka 45 ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Rais Samia alisema anatambua Jeshi la Polisi limeunda kamati ya uchunguzi lakini ameagiza iundwe kamati hiyo huru ili ikafanye uchunguzi wa mauaji ya Mtwara yaliyofanywa na askari polisi. Mauaji ya Mtwara yalitokea Januari 5, mwaka huu na mauaji ya Kilindi yaliyotokea Januari 30, mwaka huu.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, kamati hiyo ina maofisa wenye dhamana kutoka mamlaka tofauti za serikali ikiwamo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ofisi ya Rais - TAKUKURU, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Waziri Mkuu pia amemwagiza Inspekta Jenerali wa Polisi, Simon Sirro awasimamishe kazi maofisa wa Jeshi la Polisi wa Mtwara na Kilindi ili kupisha uchunguzi wakati timu aliyoiunda ikifanya kazi yake.

“Viongozi hawa wanapaswa wakae pembeni, watahojiwa na hii timu wakiwa nje ya ofisi,” aliagiza Waziri Mkuu na kuwataja maofisa hao kuwa ni Kamanda wa Polisi (RPC) Mkoa wa Mtwara, Mkuu wa Upelelezi wa Mkoa (RCO) wa Mtwara na Mkuu wa Kituo cha Polisi Mtwara cha eneo alilofia mfanyabiashara Mussa Hamisi na Mrakibu Msaidizi wa Polisi, Greyson Mahenge, anayedaiwa kujinyonga.

Waziri Mkuu pia aliagiza Kamanda wa Polisi wa Wilaya ya Kilindi na Ofisa Upelelezi wa Wilaya wakae pembeni kupisha uchunguzi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Juhudi za pamoja zinatakiwa kudhibiti ongezeko la saratani

**TAARIFA** mpya zilizotolewa kuhusu ugonjwa wa saratani, zinaonyesha kuwa tatizo hilo bado ni kubwa na kasi inaongezeka hatua ambayo inaashiria maelfu ya watu kuendelea kupoteza maisha.

Katika taarifa hiyo, imebainika kuwapo kwa wagonjwa wapya 42,060 kwa mwaka huku 28,610, sawa na asilimia 68 wakifariki dunia kutokana na maradhi hayo. Taarifa za mwaka 2021 zilizotolewa na Taasisi ya Saratani Ocean Road, zinaonyesha aina za saratani zinazoongoza, kwa wanaume ni tezi dume na wanawake ni ya mlango wa kizazi.

Pia taarifa zinabainisha kwamba kwa wanaume saratani zinazowaathiri zaidi ni pamoja na tezi dume kwa asilimia 21, saratani ya koo asilimia 11.8, saratani ya utumbo mkubwa na mdogo asilimia tisa na saratani ya mdomo na kinywa asilimia 7.3.

Kwa upande wa wanawake, saratani zinazowaathiri zaidi ni pamoja na saratani ya mlango wa kizazi asilimia 43, saratani ya matiti asilimia 14.2 na saratani ya koo asilimia 3.8.

Akitoa tamko la Siku ya Saratani Duniani juzi, Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, alisema katika miaka 10 iliyopita, Tanzania imeshuhudia ongezeko kubwa la wagonjwa wa saratani huku akibainisha kwamba chanzo kikuu ni mtindo wa maisha tofauti na ilivyokuwa awali ambapo wagonjwa wengi walikuwa wale wenye saratani zinazotokana na maambukizi ya virusi.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa mujibu wa taarifa za karibuni, takwimu za Shirika la Umoja wa Mataifa la Utafiti wa Saratani (IARC) za mwaka 2018 zinaonyesha kwa Tanzania watu 76 kati ya 100,000 hugundulika kuwa na saratani.

Sababu kubwa za kuongezeka kwa ugonjwa huo ni matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, matumizi ya pombe kupita kiasi na ulaji usiofaa kama kutokula mboga na matunda, matumizi ya chumvi na sukari kwa wingi.

Kwa ujumla, takwimu hizo juu ya kasi ya saratani zinatisha si kwa maisha tu bali hata kwa ustawi na uchumi wa nchi, hivyo jitihada za pamoja zinatakiwa ili kupambana na janga hilo ambalo linaangamiza maisha ya watu kila uchao.


Ni wazi kwamba kama hatua madhubuti hazitachukuliwa, tunaweza kushuhudia ongezeko la wagonjwa na vito kutokana na ukweli kwamba watu wengi wamekuwa wakifika katika vituo vya kutolea huduma za afya wakiwa katika hatua za mwisho za ugonjwa husika. Kwa mantiki hiyo, watu wahamasishwe kupima afya mara kwa mara na kuwapo kwa mpango maalum wa kutoa matangazo juu ya watu kwenda kufanyiwa uchunguzi wa afya mara kwa mara. Pia uanzishwe mpango maalum wa kuwafikia wananchi katika maeneo ya vijijini hususan katika mikoa ile ambayo kuna maambukizi makubwa ya ugonjwa huo.

Kama alivyoshauri Waziri Ummy, ni vyema ikatengwa siku maalumu kila mwezi kwa ajili ya kupima saratani kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na uchunguzi.

Hatua hiyo itawezesha watu kujitokeza na kupima ili kujua afya zao na hatimaye kuchukua hatua. Pamoja na hayo, inatakiwa kutolewa elimu ili kuongeza uelewa kwa jamii. Mfano wa elimu inayotakiwa ni kuwa na vipindi vya kuelimisha watu kuhusu saratani, athari zake na njia za kujikinga kama ilivyokuwa katika elimu na kampeni za kupambana na UVIKO-19.

Yote haya yanawezekana iwapo kila mdau kwa nafasi yake atafanya yale yanayompasa. Pia kuwe na ujumbe unaotoa elimu juu ya saratani kama ambavyo imekuwa ikifanyika kwa magonjwa hatari kama Ukimwi na Corona. Serikali isiachiwe jukumu hilo peke yake pamoja na taasisi zake bali asasi za kiraia hasa zinazojihusisha na masuala ya afya zishiriki kikamilifu katika jambo hilo na kwa kufanya hivyo kutakuwa na mafanikio makubwa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kaya maskini hewa za TASAF ni kikwazo kwa maendeleo ya jamii

Na Sabato Kasika

**KUWAPO** kwa Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (Tasaf), kunalenga kupunguza tatizo la umaskini kwa familia zinazotoka katika kaya zisizojiweza.

Kaya hizo ni zile zinazotajwa kuishi katika umaskini uliotukuka, ambapo njia mojawapo ya kuzinusuru ni kutumia mpango huo ili kubadili maisha ya wanufaika kwa kuwajengea uwezo wa kuanzisha vitega uchumi.

Hatua hiyo pia inalenga kuwafanya wasiwe tegemezi, badala yake wawe na uwezo wa kujitegemea kiuchumi na kukidhi mahitaji yao ya msingi kuanzia chakula, mavazi, malazi, makazi na mengine yote.

Matarajio ya kuanzishwa kwa mpango huo, ni kuona wanufaika halali wanafikiwa na mradi huo, lakini kumekuwapo na malalamiko yanayoripotiwa katika vyombo vya habari kuwa baadhi yao hawafikiwi.

Kwamba baadhi ya watendaji waliokabidhiwa kusimamia mpango huo hufanya undanganyifu na kusababisha kuwapo kwa idadi kubwa ya kaya maskini hewa na hata wanufaika wake huwa si wale waliokusudiwa.

Tuhuma hizo zimewahi kuthibitishwa na baadhi ya viongozi wa serikali na kutaka waliopewa dhamana hiyo kuhakikisha wanafanya kazi yao kwa weledi ili kila mlengwa anufaike badala ya kuwapo kaya maskini hewa.

Kuwapo kaya maskini hewa, ni wazi zinaweza kuwa ni hujuma kwa taifa, hivyo ingekuwa ni vyema kama wahusika wataepuka kujihusisha na mipango hiyo kwa kukwamisha kile ambacho serikali inakifanya kwa wananchi wake. Ninaamini kwamba, Mtanzania mwenye kiu ya maendeleo ya nchi yake, hawezi kufurahia mtindo huo kuwapo kaya maskini hewa ambazo kimsingi zinaweza kuchangia kuendelea kuwapo kwa umaskini katika jamii.

Ikumbukwe kuwa fedha za umma zina majukumu mengi na inawezekana ndiyo maana mwaka 2000 serikali ikapata udhamini wa Benki ya Dunia (WB), ili kusaidia mpango huo wa kunusuru kaya maskini.

Ni vyema kila mmoja akatambua kuwa serikali inatumia fedha hizo pia kutekeleza miradi yenye lengo la kuchochea maendeleo ya uchumi hasa miundombinu ya usafiri, nishati ya umeme katika maeneo ya vijijini.

Lakini pia asilimia kubwa ya kaya maskini wanaishi vijijini, hivyo kunakuwapo kaya hewa maskini ni wazi inakuwa ni sawa na kuwazibia riziki walengwa na kuchelewesha ukamilishwaji wa miradi ya maendeleo yenye tija kwa umma.

Hivyo, ni vyema kuhakikisha kaya maskini hewa zisiwe na nafasi katika mpango huo ili kubakiza zenye sifa na vigezo ili kupunguza ukubwa wa umaskini katika jamii na taifa kwa ujumla.

Pamoja na hilo, jambo lingine ambalo limekuwa likilalamikiwa na baadhi ya walengwa, kwamba wasimamizi wa malipo waliopendekezwa na wanufaika, huwa hawawafikishii kiasi cha fedha kinachotolewa na Tasaf kila mwezi.

Badala kufikisha fedha ili zitumike kama zilivyokusudiwa, inadaiwa kuwa baadhi yao huchukua na kufanyia mambo yao na kuwaacha babu au bibi wakiendelea kuhangaika bila chochote.

Hiyo inatoa taswira kuwa, ndani ya familia pia kuna changamoto inayohitaji kufanyiwa kazi, ili kuwapunguzia kero wanufaika wa mpango huo kuliko kuwaacha wajukuu au watoto wakiwadhulumu babu, bibi, mama au baba.

Kitendo hicho cha watoto au wajukuu kujinufaisha na fedha za wazazi wao kinawakosesha haki yao walengwa kupata kile kilichokusudiwa na pia kinakwamisha juhudi za serikali kukwamua kaya maskini.

Serikali inataka kubadili maisha ya wanufaika na kuwajengea uwezo wa kuanzisha vitega uchumi na kuwafanya wasiwe wategemezi, hivyo ni vyema wanaokwamisha juhudi hizo wakachukuliwa hatua za kisheria.

## KWA MASLAHI YA TAIFA

# Hongera 'Idara' kuhudumia wastaafu wake hadi mwisho



Na Pascal Mayalla

NIMEITAJA 'Idara' tu bila kumalizia ili andiko hili liwe ni idara yoyote na si lazima ile idara tu.

Ushujaa ni kitendo cha kufanya jambo kubwa kwa taifa lako. Mashujaa hawa wako wa aina mbili, mashujaa wa wazi (open heroes) na mashujaa wa kimya (silent heroes"). Mashujaa wa wazi ni wale wanaotambulika na kutambulishwa rasmi kuwa ni mashujaa, kama wale wa majeshi yetu - Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Polisi, Uhamiaji, Magereza na Zimamoto, ambao huvishwa nishani za ushujaa waziwazi huku vyombo vya habari vikialikwa. Mashujaa wa kimya wenyewe pia wanavishwa nishani lakini kimya kimya.

Jana, Februari 5, 2022, katika kijiji cha Uparo, Kirua Vunjo, Moshi mkoani Kilimanjaro, mmoja wa mashujaa hawa wa 'Idara' kwa jina la Graciana Morris Kundi, alihifadhiwa katika nyumba yake ya milele baada ya kufariki dunia akiwa na umri wa miaka 85.

Kutokana na unyeti wa 'Idara', japo sijui Graciana Morris Kundi alikuwa kitengo gani na alifanya ushujaa gani, mwaka 1985 alitunukiwa nishani na Rais wa Kwanza wa Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere kisha mwaka 1991 akatunukiwa tena nishani nyingine na Rais (mstaafu) Ali Hassan Mwinyi.

Graciana Morris Kundi, alizaliwa Septemba 30, 1936 katika kijiji cha Iwa Kirua Vunjo. Mwaka 1944 hadi 1949, alipata elimu ya msingi katika shule ya Iwa. Mwaka 1950 hadi 1954, aliendelea na masomo ya sekondari Ndala, Kipalapala mkoani Tabora na mwaka 1955 hadi 1958 akajiunga na Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Tabora.

Mwaka 1960 alijiunga na Chuo cha KNCU kusomea kozi ya 'Stenograph' na mwaka 1961, aliajiriwa rasmi serikalini na kufanya kazi hadi kustaafu mwaka 1992, akiwa amelitumikia taifa kwa miaka 41. Baada ya kustaafu, alirudi kijijini, Kirua Vunjo na kuishi maisha ya kawaida hadi mauti yalipomkuta, Jumatano Februari 2, 2022 kwa kufa akiwa usingizini.

Nimeipongeza 'Idara' kwa kundelea kuwajali watumishi wake wastaafu miaka yao yote ya maisha yao hadi kifoni kwani baada ya kupokea taarifa ya kifo hicho, maofisa wa 'Idara' walifika nyumbani na kutoa rambirambi nene.

Kama nilivyosema, sikuujua ushujaa wa mama huyu zaidi ya kuvishwa mishani na marais Nyerere na Mwinyi. Kikawaida, katika majeshi, wanaovishwa nishani ni maofisa wa ngazi za juu. Wale maofisa wa ngazi za chini, huvishwa nishani na wakuu wa vikosi vyao. Hivyo Graciana Morris Kundi, atakuwa ni alikuwa ofisa wa juu wa 'Idara'.

Kwa vile nimetokea kufahamu kiwango cha pensheni alichokuwa akilipwa na kwa vile nayafahamu mafao ya kisasa ya viongozi wakuu wanapostaafu, hulipwa asilimia 80 ya mshahara wa ofisa aliye madarakani au kazini, hivyo ukisikia kiwango wanacholipwa wastaafu hawa wa zamani, waliolitumikia taifa maisha yao yote na miaka yao yote, kama ni mtu wa machozi ya karibu, unaweza kulia.

Kama maofisa wa juu wa sasa wana mafao manene, manono, hata wastaafu wa zamani, wana haki ya pensheni zao zipangwe kwa asilimia ili mishahara ya ofisa wa ngazi yake ikipanda, na wastaafu pia pensheni zao zipande. Mwalimu Nyerere aliamini katika falsafa ya binadamu wote ni sawa na baada ya kuwa Rais wa Tanzania, akakuta jinsi mshahara wake ulivyokuwa juu kulinganisha na wengine, alijipunguzia ili kujenga usawa.

Kama ni kweli binadamu wote ni sawa, maofisa wa ngazi zote za serikali wanapaswa kuwa sawa na wanastahili kutendewa sawa. Iweje maofisa wakuu tu ndio wanajipangia mafao manene, manono ya kustaafu kwa kiwango cha asilimia 80 ya ngazi husika, halafu wastaafu wengine, wanalipwa mafao kiduchu ajabu?

Pia kama ni kweli tunamuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Nyerere kwenye usawa wa binadamu, tumuenzi kwa vitendo na si kwa maneno tuu. Maofisa wote wa serikali, wanapaswa kutendewa haki sawa kwa wote na si haki kwa maofisa wakuu tu halafu wengine kuachwa kupambana na hali zao.

Nimeipongeza 'Idara' kwa kuwajali wastaafu wake si tu kwa kuendelea kuwalipa mishahara (japo kiduchu), maisha yao yote, bali kwa kuwajali si tu katika uhai, bali hadi kifoni.

Swali ni kwa nini ni baadhi tu ya wastaafu na si wote?. Wastaafu wengine wanaojaliwa na serikali kifoni ni majaji wastaafu, na si mahakimu au watumishi wengine wa mahakama. Swali ni kwa nini, baadhi tu ndio wajaliwe hadi kifoni, lakini wengine waachwe wajifie na hali zao?

Watu wanapojiunga na idara fulani ya serikali na kuitumikia serikali maisha yao yote hadi kustaafu, kitendo tu cha kufanya kazi serikalini maisha yao yote na viwango duni vya mishahara ya serikali, hilo pekee tu ni ushujaa. Kwa mantiki hiyo, watumishi wote wastaafu wa serikali ni mashujaa wa kimya.

Kama walijitoa kuitumikia serikali maisha yao yote, japo wanalipwa pensheni kiduchu, inapofika kifoni, serikali inyooshe mkono wake kuwajali katika safari yao ya mwisho.

Kuna msemo usemao, mtoto wa nyoka ni nyoka, hivyo kwa watu wanaonifahamu mimi Pascal Mayalla, kama mwanahabari jasiri, asiyeogopa, kumwuliza kiongozi yoyote swali lolote, ujasiri huo nimeurithi kutoka kwa 'Silent Hero' huyu, Graciana Morris Kundi, kwa sababu huyu ni mama yangu mzazi.

Kwa niaba ya Familia ya Shujaa huyu Graciana Morris Kundi, tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wote walioshiriki na sisi katika kipindi hiki kigumu cha kumpoteza mama yetu. Tunawashukuru sana wote walioshiriki katika kutoa michango na kufanikisha msiba na mazishi bilas kuwasahau ndugu jamaa na marafiki.

Kipekee tunawashukuru madaktari wa hospitali za KCMC, Faraja na St. Monica pamoja na serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania kwa kuendelea kumtunza hadi mauti yalipomkuta.

Mama yetu Graciana Morris Kundi, amepigana vita vilivyo vizuri, mwendo ameumaliza, imani ameilinda. Bwana ametoa, Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe. Lala salama Mama Graciana Morris Kundi (Mama Pasco).

**Wasalaam.**

## MADONGO YA MGAGAGIGIKOKO

# Zinasikika kelele za 'tunataka Bunge Live'!



Na Joseph Kulangwa

**Alichokiona na kukifikiria ndicho kilichomfanya akakosa goli ambalo mtazamaji au mshangiliaji alidhani ingekuwa rahisi tu kuubutua na kuingia langoni, hata kama angetumia mgongo.**

UKIANGALIA mchezo wa mpira wa miguu, ambao wengine huuita soka au kabumbu, utadhani ni rahisi sana kuucheza kwa sababu ni kiasi cha wewe kulenga mguu na kupiga teke ukaenda mbele.

Ni kweli ni rahisi kufanya hivyo, hata kama unapiga kuupeleka kusini, kaskazini, mashariki au magharibi au juu, ni ilimradi usonge mbele utoke uliko uende kwingine.

Na kama kuna magoli pande mbili za uwanja, lazima uupige uende kwa adui yako, yaani upande wa pili ili kupata ushindi kwa sababu mchezo huo mwishowe huhakikisha mshindi anapatikana.

Ndiyo sababu kila mwenye timu yake, hupenda kuona ana golikipa mzuri lakini pia ana mfungaji mzuri kwa sababu hatimaye magoli mengi ya kufunga ndiyo hutoa mshindi na ya kufungwa hutoa mshindwa.

Hakuna anayekubali kushindwa ng'o kwa sababu hatima yake ni zawadi kwa mshindi na si kwa mshindwa. Hivyo mtazamaji anaweza asijue kuucheza mpira lakini akajua kumwelekeza mchezaji nini la kufanya.

Ndiyo sababu mfungaji akishindwa kufunga utasikia shabiki anasema hapo hata angesukuma kwa kifua lilikuwa goli lakini hajui kuwa mfungaji huyo alikuwa katika hali gani na alikuwa anaona nini alipotaka kufunga.

Alichokiona na kukifikiria ndicho kilichomfanya akakosa goli ambalo mtazamaji au mshangiliaji alidhani ingekuwa rahisi tu kuubutua na kuingia langoni, hata kama angetumia mgongo.

Hali hiyo hujitokeza kwa hata mchezaji wa ndani ambaye anapokuwa ndani hujishangaa kwa nini anashindwa kutumia nafasi anayoipata kufunga magoli na kujilaumu au kujishangaa.

Lakini anapotolewa nje ya uwanja akakaa benchi, hujikuta naye akaona kama alivyokuwa aonavyo mtazamaji kwamba kumbe pale angejipanga sawa na goli bila shaka angetikisa nyavu. Hiyo ni baada ya kukaa nje na kujitafakari.

Hata katika maisha ya uongozi, mambo haya hujitokeza. Mtu anaweza kuwa na nafasi fulani ya uongozi na kukaa ofisini mkamshagaa mbona hafanyi vyema kama alivyokuwa kabla, akiwa nje ya uongozi!

Mnaweza kumwona alikuwa msemaji sana vijiweni, akikosoa na kusema na kuelekeza lakini inapofika nafasi yake ya kukalia kiti kile alichokuwa akikisema na kukielekeza, mnaona kabisa amepwaya.

Tunaona hata katika nafasi zetu za mawaziri wetu hawa, mkubwa mmoja anaweza kuwatazama akaona pengine hawamfai au hawamsaidii, akaamua kuwaondoa kwa lugha ya kuwatumbua au kutengua nafasi zao.

Wakakaa nje ya ulingo na kutazama mchezo na kuona pengine walikuwa mbona wanafanya kama hao walioingizwa, lakini bado tu uamuzi wa kocha ni kuwatoa, akidhani ama wanafanya uzembe au kiwango kimeshuka.

Lakini inawezekana maelekezo ya kocha ndiyo wakati mwingine yakamsababisha mchezaji huyo yaani Waziri, akashindwa kufanya vyema, hivyo kupumzishwa, ili aangalie wenzake wanafanya nini.

Bila shaka wazo langu linatua kwa kijana wa Moses Nnauye. Alikuwa mchezaji mzuri tu katika timu ya JPM lakini katika kutaka kuonyesha anafunga magoli kivipi, akajikuta anamkwatua 'straika' Paulo. Kocha akamtemelea mbali.

Mi najua chenga zingine alizokuwa anapiga dogo huyo kwa ajili ya kutaka kumwonyesha Kocha kuwa anaupiga mwingi, baadaye ikaonekana mbwembwe zake haziendani na anachotaka Kocha. Ndiyo sababu akatemwa.

Lakini ikafika wakati Kocha naye akaondoka, akaja Kocha mwingine, akaona kiungo huyu bado wamo, ngoja nimrudishe tuone tena kama kiwango kiko pale pale.

Mi naona anaupiga mwingi kiungo huyu, alipoanza tu na 'DSTV' nikaona hapa mabao hayakosekani, kama ya yule 'straika' wa DRC anayetetema huyu naniliu huyu sijui nani wanamwita sijui Manini vile. Nimemsahau.

Mchezaji ukimpa nafasi acheze na ukampanga katika nafasi ananyoimudu, lazima akuoneshe kiwango na kipaji alichonacho n kupe matokeo. Nape yuko hivyo kwamba akipewa fursa ataiendea haki na haki ikaonekana imetendeka.

Najua anapiga jaramba katika kuhakikisha Watanzania wananufaika na anachokisimamia ndiyo sababu kwa mbali nasikia kelele za kuwa watu kutaka Bunge mubashara au 'Bunge Live'.

**Nape upo? Alamsiki!**

## KONA YA UKWELI

# Wagombea uspika vyama hivi wanajimaliza kisiasa



Na Thobias Mwanakatwe

Hoja yangu kwa leo ni kuhusu wagombea wa vyama vya upinzani walioingia kwenye kinyang'anyiro hicho kama kweli walikuwa 'serious' au walikuwa wanaleta mazingaombwe tu katika kuwania nafasi hiyo nyeti ya mhimili wa dola uliopewa dhamana ya kutunga sheria.

FEBRUARI Mosi, 2022 historia nyingine iliandikwa baada ya Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kumchagua Dk.Tulia Ackson kuwa Spika wa Bunge hilo, Dk. Tulia anakuwa mwanamke wa pili kuchaguliwa kuwa Spika katika historia ya Tanzania. Mwanamke wa kwanza alikuwa Anne Makinda kuanzia mwaka 2010 hadi 2015.

Katika uchaguzi huo, Dk. Tulia aliwabwaga wagombea wenzake wanane wanaotoka vyama vingine vya siasa kwa kupata asilimia 100, baada ya kujizolea kura zote 376 zilizopigwa.

Ushindi huo ni wa kihistoria kulinganisha na aliowahi kuupata mtangulizi wake Job Ndugai ambaye alichaguliwa kuwa Spika wa Saba wa Bunge la Tanzania tangu uhuru, kwa kupata kura 254 dhidi ya kura 109 za mshindani wake wa karibu, Goodluck Ole Medeye kutoka Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA).

Wagombea wa vyama vingine waliobwagwa na Dk.Tulia ni Abdullah Mohammed Said (NRA), Mhandisi Aivan Maganza (TLP), David Mwaijojele (CCK), Georges Busungu (ADA -TEA), Kunje Ngombale Mwiru (SAU), Maimuna Said Kassim (ADC), Ndonge Said Ndonge (AAFP), Sadoun Khatib (DP).

Uchaguzi wa Spika mpya wa Bunge umefanyika kutokana na aliyakuwa akishika nafasi hiyo, Job Ndugai, kujiuzulu baada ya kutokea mvutano mkubwa wa kisiasa.

Sababu kubwa ni kutokana na kauli yake aliyoitoa kuhusu hatua ya Rais Samia Suluhu kukopa Sh. trilioni 1.3. Ndugai alinukuliwa na vyombo mbalimbali vya habari akisema kuna siku Tanzania itapigwa mnada kutokana na mikopo mikubwa inayoendelea kuchukuliwa na serikali.

Hoja yangu kwa leo ni kuhusu wagombea wa vyama vya upinzani walioingia kwenye kinyang'anyiro hicho kama kweli walikuwa 'serious' au walikuwa wanaleta mazingaombwe tu katika kuwania nafasi hiyo nyeti ya mhimili wa dola uliopewa dhamana ya kutunga sheria.

Niliona baadhi ya wagombea wa kiti hicho cha uspika kama vile walikuwa wanaleta utani. Hili lilijidhihirisha wakati wakijieleza mbele ya wajumbe ambao ni wabunge ili kuwashawishi wawapigie kura.

Katika kile ambacho nimekiona ni kutokuwa 'serious' kwa wagombea hawa, mfano mmoja wao alinukuliwa akisema suala la kugombea uspika lilikuwa suala la ghafla kwake kwa kuwa alikuwa safarini mikoani.

Mwingine akajieleza kuwa akichaguliwa kuwa Spika atapunguza idadi ya vikao vya bunge lakini ataongeza posho kwa wabunge.

Hizo ni baadhi tu ya kauli za wagombea ambazo kimsingi zinaleta kichefuchefu na kuonyesha tulivyo na safari ndefu kwa vyama vya upinzani ambavyo nadiriki kusema baadhi ya wagombea wao hawako 'serious' kabisa.

Kutokuwa makini kwa wagombea hao katika kuwania nafasi nyeti za uongozi ndiko kumewasababisha Watanzania kutokuwa na imani kabisa na vyama vya upinzani katika nchi hii.

Mizaha inayofanywa na baadhi ya wagombea wa vyama hivi, kimsingi inavigharimu hata vile ambavyo vinaonekana kuwa 'serious' kuendesha siasa za upinzani kutokana na wananchi kuanza kutafsiri kuwa ni wale wale.

Hatua hii naweza kusema wagombea wa vyama hivi kutokana na mizaha na kutokuwa makini katika kuwania nafasi nyeti za uongozi kunavisababisha vyama hivyo kupoteza mwelekeo na umaarufu kama sio kujimaliza kabisa kisiasa.

Kutokana na vyama hivi kutokuwa na watu makini wa kugombea ndiko kunazidi kukipa mailegi Chama Cha Mapinduzi (CCM) kushika hatamu za nafasi mbalimbali za uongozi katika nchi.

Unapowadia uchaguzi mkuu, nimekuwa nikishangazwa sana ninapoona wagombea wa vyama fulani wanasema uchaguzi haukuwa huru na wa haki, wameibiwa kura. Hivi unawezaje kusema hivyo kama unakuwa na wagombea kama hawa tuliowaona kwenye kinyang,anyiro cha uspika halafu utegemee kushinda?

Nafahamu wagombea wa vyama hivyo walitumia nafasi yao ya kikatiba kugombea lakini basi wasionekane vituko wajaribu kuwa serious na mambo ya msingi vinginevyo wananchi watakuwa hawawaelewi kabisa.

Hivi sasa ukipita vijiweni na maeneo mbalimbali ukasikia maneno ya wananchi kuhusu vyama vya upinzani hakika wahusika wa vyama hivi wangekaa chini na kujitafakari wabadilishe upepo wa kufanya siasa vinginevyo wataendelea kuwa wasindikizaji katika chaguzi mbalimbali zijazo.

Ukiangalia kwa kifupi kazi za Spika ni kwamba yeye ni kuratibu shughuli na majadiliano ya bunge.

Huamua juu ya maswali ya utaratibu bungeni, ufuatano wa wabunge katika majadiliano , kutangaza matokeo ya kura bungeni na kadhalika. Ndiye mwakilishi wa bunge kwa ujumla.

Kama majukumu ya Spika ni kama hayo fikiria kama tunafanya kosa anachaguliwa Spika ambaye hayuko makini kama baadhi ya wale niliowaona wakijinadi, Bunge litakuwa vipi kuwa na Spika wa aina ile? Hii ni aibu kwa nchi kuwa na wagombea wa dizaini ile.

**Kwa maoni na ushauri tumia barua pepe mwanakatwe2005@yahoo.co**

## DARASA LA NDOA

# AMANI NI MSINGI, CHACHU YA MAFANIKIO KATIKA NDOA



Na Mch.Dk. Enock Mlyuka

KUNA mawmo usemao amani ndiyo msingi wa maendeleo katika jamii. Ni ukweli usiopingika kwamba bila kuwa na amani, hakuna jambo lolote litakalofanyika kwa ukamilifu na mafanikio.

Hivi sasa tunaishi katika jamii inayobadilika na inayotupa wajibu wa kuendelea kukumbushana kuhusu suala la ujenzi wa jamii inayosimikwa katika msingi wa haki, amani na utulivu kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya taifa. Haki na amani ni mapacha wasiotengana. Haki inahusika zaidi katika kuleta amani na uhusiano mzuri kati ya mwanadamu, kati ya mwanadamu na uumbaji na kati ya utamaduni mbalimbali. Hivyo, tunda la haki ni amani. Mahali penye amani hutazamiwa kuwa na utulivu.

Kama tunavyofahamu, haki ni suala mtambuka lenye kubeba mambo mengi. Watu wana haki ya kuishi na kuwa na maisha mazuri yenye heshima na nidhamu; haki ya kulindwa katika maisha yao; haki ya kushiriki katika shughuli za maendeleo;haki ya kumwabudu Mungu kadiri ya imani na dhamira zao; haki ya kuchagua hali ya maisha wanayoyapenda zaidi;haki ya kuchagua viongozi wanaowataka; haki ya kuwa huru katika kutafuta ukweli.

Siku zote haki huenda pamoja na wajibu na upendo. Haki pasipo upendo na kuwajibika ni unafiki na dalili ya kukaa ndani ya kifo. Amani ni moja ya matunda ya haki na zawadi kutoka kwa Mungu inayomwajibisha binadamu.

Amani ni msingi wa wema, heshima na maendeleo endelevu na fungani ya binadamu. Kwa mantiki hiyo, amani ni zawadi inayopaswa kutunzwa kwa njia ya kuwa na ndoa imara na malezi yenye dhamira nyofu kwa kulinda na kuheshimu utu wa binadamu, ustawi na maendeleo ya familia, jamii na taifa.

Kwa hiyo, watu wanapooa na kuolewa wanapaswa kujizatiti katika ujenzi wa jamii inayosimikwa katika msingi wa haki, amani na utulivu kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya familia, jamii na taifa. Wanandoa wafahamu nafasi na wajibu wao katika ndoa na kuepuka vitendo vya unyanyasaji na ukatili ndani ya ndoa.

Wanandoa wanao wajibu wa kujifunza ili kufahamu misingi na madai ya taasisi ya ndoa kwa kuwa ndoa ni shule ambayo haina kuhitimu. Kila siku wanapaswa kujifunza na kukua katika ndoa.

Kimsingi, jamii inatazamia kuona ndoa bora na siyo bora ndoa kwani ndoa ni msingi na kitovu cha malezi na familia.

Ndoa zikiwa imara, tutakuwa na familia imara; familia zikiwa imara, tutakuwa na jamii imara; tukiwa na jamii imara, tutakuwa na taifa imara. Maendeleo ya taifa yanategemea uwapo wa ndoa imara kwani katika ndoa ndiko rasilimali watu inakotengenezwa. Watu ni rasilimali muhimu na bila watu hakuna taifa wala maendeleo.

Ndoa zikiwa imara, haki, amani, utulivu na maendeleo vitaendelea kuwapo katika jamii. Umefika wakati sasa badala ya wazazi, ndugu na jamaa kujikita pekee katika kuandaa sherehe kubwa za harusi ni muhimu sana kuelekeza nguvu katika kuwaandaa vijana wetu wa kike na kiume ili wawe wake na waume bora.

Vinginevyo, tutakuwa tunandaa sherehe kubwa za harusi za ndoa zisizodumu, hali inayoathiri mtu kisaikolojia, kiafya, kimwenendo, kiroho na kiuchumi. Athari hizi hasiwahusu vijana waliofunga ndoa tu, bali watoto waliozaliwa katika ndoa hizo na wazazi ambako wanandoa hao wanatoka.

Ni wazi kwamba ndoa bora ni kielelezo cha hali ya juu kabisa cha upendo katika jamii; matunda ya ukomavu yanayohitajika katika ujenzi wa familia, uvumilivu, uaminifu na bidii.

Kamwe tofauti za haiba (personality dynamics) kisiwe chanzo cha vurugu na mpasuko katika ndoa, kwani hali hii inaweza kuangamiza ustawi wa familia na maisha ya wanandoa wenyewe.

Wanandoa wanapaswa kufahamiana vizuri, kuheshimiana na kuchukuliana katika tofauti na kasoro walizo nazo ili kulinda utu, heshima na haki za binadamu.

Wazazi wamebeba dhamana kubwa ya malezi ya watoto wao. Wazazi wanao wajibu wa kulea watoto wao katika njia ipasayo na kuweka misingi bora ya maisha yao ya baadaye. Wahenga wanasema, mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo. Kwa hiyo, ili kuweza kutimiza wajibu wa malezi bora, wazazi wenyewe wanapaswa kuwa kielelezo cha tabia njema na nidhamu.

Kutenda haki ili kutunza amani na utulivu katika ndoa ni wajibu wa kila mwanandoa. Hivyo, watu wanapoingia katika ndoa, mume na mke wafahamu kuwa wanao wajibu wa kuhakikisha kuwa nyumba yao inakuwa kisiwa cha amani na utulivu na siyo kuwa uwanja wa fujo na visasi. Yote yatawezekana iwapo kila mwanandoa atatimiza wajibu wake na kumtanguliza Mungu.

**■Dk. Mlyuka ni Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania Marriage and Child Care Foundation (TaMCare), asasi inayojishuhulisha na masuala ya ndoa, familia na malezi. Kwa maelezo zaidi, tembelea www.tamcare.or.tz.**

**Fuatilia mafunzo zaidi katika tamcaretv online. Kwa maoni na ushauri wasiliana naye kwa: info@tamcare.or.tz au +255744000066.**

# MAISHA

FEBRUARI 6, 2022

Nipashe


Baba, Mama na Mwana

*Jumapili*




Ukurasa 14


## Namna Kuku anavyopikwa



Ukurasa 15

## MAISHA NI NYUMBA

Hivi ndivyo unapaswa kusafisha sofa




## KATUNIKA

Ukurasa 16





# HUJAKOSEA KUVAA SATINI

## Mng'aro wake si mchezo

Ukurasa 13


MAJIBU YA WIKI ILIYOPITA









## AMSHA AKILI




## TOA TOFAUTI 5




## FUMBO TOTO



Jaza maneno yafuatayo katika vyumba vilivyopo wazi:
BEI, ANA, TENGA, KWETU, TWANGA, KWENYE

## WATOTO

# PAKA RANGI




## CHEKA



**Alichokifanya daktari**

MTOTO Juma alikuwa akimsaidia mama yake kupalilia bustani yao ya maua. Wakati wakiendelea na kazi hiyo, Juma alimgeukia mama yake na kumuomba kumuuliza swali.

Juma: Eti mama naweza kukuuliza?

Mama: Uliza tu mwanangu

Juma: Mama eti marehemu huwa anapata matibabu kama watu waliokuwa hai?

Mama: Hapana ila tunawazika ili Mungu awalaze sehemu nzuri

Juma: Mbona mwalimu ametufundisha kwamba Sikio la kufa halisikii dawa?

Mama: Mwalimu wenu hakukusudia watu waliokufa, bali alikuwa na maana kwamba kitu chochote kinapofikia mwisho. Huwezi kuzuia kisiharibike.

**SWALI**
Mlima Kilimanjaro upo mkoa gani wa Tanzania?

## MAISHA NDIVYO YALIVYO

Na Flora Wingia



# Unajua moyo wa mwanadamu ni kichaka?

KARIBU msomaji wangu tuendelee kuelimishana kuhusu maisha yetu yalivyo. Wiki mbili mfululizo nimejadili sana hatari ya mtu kufa ndani yake. Nikasema ili ujiuje kuwa umekufa ndani, jichunguze nafsi yako.

Leo nigeukie moyo wa mwanadamu. Unapotaja moyo wa mwanadamu unakuwa umetaja au kugusa kiungo muhimu katika mwili. Kwa namna moja au nyingine tunaweza tukasema moyo ni injini katika mwili wa mwanadamu.

Kama vile gari lisilokuwa na injini haliwezi kwenda, vivyo hivyo na mwanadamu moyo wake ukiwa na hitilafu, mwili mzima utakuwa na maumivu. Wakati mwingine hata kupelekea kupoteza maisha.

Leo nizame zaidi kujadili moyo katika anga la kiungu. Mungu katika moja ya maandiko yake anasema: “Maandalio ya moyo ni ya mwanadamu, bali jawabu la ulimi latoka kwa BWANA”.

Sasa unaweza kuuliza, kwa nini moyo wa mwanadamu ni kichaka? Kuwa tayari kukubali au kuamua kitu ni kwa mwanadamu mwenyewe. Na kuamua kufanya baya ni mwanadamu mwenyewe ameamua. Yeye ndiye anayeandaa kufanya lile atakalo kulifanya.

Jiulize, moyo wako, injini ya mwili wako inaamua nini. Umekubali nini, uko tayari kufanya nini, una maandalizi gani mwaka huu 2022? Bila shaka, hapa hakuna hata mmoja anayesema mimi nimekwenda tu kwa sababu ni tangazo fulani limetolewa.

Kila mmoja ndani ya moyo wake ana kusudi, ana maono, ana maandalizi ya kitu fulani kwa ajili ya maisha yake. Neno la Mungu linasema, “moyo ulio mzima ni uhai wa mwili, bali husuda ni ubovu wa mifupa”.

Moyo ulio mzima unasababisha afya kwenye mwili wako. Lakini husuda ni tatizo! Husuda kwa lugha nyepesi ni wivu. Siyo siri kwamba wivu umesababisha watu wengi kupata madhara wao wenyewe au kuleta madhara kwa wenzao bila hatia.

Tumeona watu wengi leo wamepata matatizo hata wengine kupoteza maisha. Yote hayo yakisababishwa na moyo wa mtu mmoja uliojaa chuki. Au kuwa na wivu pengine kwa jambo lile zuri alilo nalo. Au pengine ni kwa nini huyu awe na kingi kuliko yeye.

Kwa mantiki hiyo, madhara yanampata yule mtu kwa sababu tu ya moyo wa mtu fulani mwenye wivu juu ya kile alicho nacho mwenzake. Lakini pia inawezekana siyo tu yule apate madhara kwani hata yeye aliyeona wivu madhara yakamkumba.

Kwa hiyo, madhara hayawezi yakaishia kwa mtu mmoja bali yakamkumba yeye aliyeyakusudia. Mtu mwenye wivu ana maumivu. Anapomuona fulani ana kitu wakati yeye hana, anaumia kwa sababu anakuwa na wivu.

Mtu huyu husahau kwamba jitihada za mtu ndizo zinazomwezeha kupata kile alichonacho kwa neema ya Mungu. Mwenye bidii ndiye anayekula lakini mvivu hawezi kula kwa sababu hakitafuti kwa jasho.

Utamuonea mwezako wivu, eti kwa nini ana nyumba nzuri, gari zuri, mke mzuri na mpole. Watoto wake wanasoma shule nzuri. Hapo huyu anayemwonea wivu mwenzie, lazima moyo wake utakuwa na maumivu.

Mungu ameweka wazi katika neno lake kwamba, “Linda moyo wako kuliko yote uyalindayo, maana ndiko zitokako chemchemi za uzima”. Kila moyo wa mtu utatoa habari zake.

Msomaji wangu, sijui wewe moyo wako una nini, je, una uzima ili kuleta uhai kwenye mwili. Moyo wako unawaza nini. Moyo wa mwanadamu ni kichaka. Huwezi kujua ndani ya kichaka kuna nini. Uko naye karibu, lakini ndani yake anatamani hata kile ulichoshika, usiwe nacho!

Inatupasa wanadamu tubadilike ndani ya mioyo yetu. Wapo watu leo wanajuta, maisha yao ni magumu kwa sababu ya husuda waliyo nayo juu ya watu wengine. Pengine ni katika ofisi zao au katika nyumba zao, wamewafanyia uharibifu watu wengine na leo maisha yao yamekuwa majuto.

Yaani hutaki mwenzako apate, na unatafuta jinsi ambavyo utamwangamiza. Hata ukimuona mwingine amesimama kwenye haki kwa ajili ya jambo fulani, pengine kutetea mtu mwingine, wewe unasimama kwa ajili ya kumuaibisha. Zaidi kushinikiza kuwa huyu hafai, hastahili ila wewe upo sahihi.

***Msomaji wangu, kama una tabia za aina hiyo, badilika ili Mungu akupe moyo mpya wa nyama kama alivyoahidi. Je, una maoni, kisa? Tuma ujumbe 0715268581.***

## NAWAZA KWA SAUTI

Na Salome Kitomari



# Ukeketaji bado ni tatizo kubwa, nguvu iongezeke

LEO ni maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kutokomeza Ukeketaji kwa Wanawake na Watoto, ambao umekuwa kikwazo kwa ustawi wa makundi hayo kisaikolojia, kiafya na kimaendeleo.

Historia ya ukeketaji imeendelea kuwapo kwa takribani karne 21 sasa. Ilipofika mwaka 2003, Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, liliidhinisha siku hiyo kila mwaka kuwa rasmi ya maadhimisho ya kutokomeza ukeketaji duniani. Nchini Tanzania, maadhimisho hayo yalianza kufanyika tangu mwaka 2010.

Tayari Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake, Watoto na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima, ametaja mikoa yenye takwimu za juu za ukeketaji nchini. Mikoa hiyo na asilimia zake kwenye mabano ni Manyara (58), Dodoma (47), Arusha (41), Mara (32) na Singida (31).

Maadhimisho haya yanafanyika chini ya kaulimbiu ya mwaka 2022 ya Kitaifa “Tuongeze Uwekezaji, Kutokomeza Ukeketaji”, ikiwa inahimiza nchi wanachama wa Umoja wa Mataifa, Tanzania ikiwamo, kuongeza uwekezaji wa rasilimali za kutosha, ili kutekeleza afua za kuzuia na kukabiliana na athari za ukeketaji. Hiyo ni pamoja na kuwabaini na kuwasaidia waathirika wa ukeketaji katika jamii.

Kwa mujibu wa taarifa ya utafiti wa Afya na Demografia ya Watu Tanzania (TDHS 2015/2016), mmoja kati ya wanawake 10 wenye umri kati ya 15 - 49 amekeketwa. Pia asilimia 35 ya wanawake hao walikeketwa kabla ya kufikisha mwaka mmoja na kwamba hali ya ukeketaji imekuwa inapungua kutoka asilimia 18 mwaka 1996 hadi 15 mwaka 2010 na 10 mwaka 2015/2016.

Waziri Gwajima alisema kupungua huku kunatokana na jitihada za serikali, asasi za kiraia na wadau wengine wanaoshiriki katika kutokomeza ukeketaji na kubadili mitizamo ya jamii kuhusu mwanamke na mtoto wa kike.

Serikali inaeleza kuwa kichocheo kikuu cha vitendo vya ukeketaji ni mila na desturi za baadhi ya makabila katika jamii, kwa kuwa unachukuliwa kama tendo la kumvusha rika mtoto wa kike kutoka utoto na kuwa mwanamke kamili, mzuri na jasiri.

Jamii inayokeketa huamini kuwa msichana aliyekeketwa anakuwa tayari kuolewa bila kujali umri wake. Mtazamo huu umepelekea ongezeko la mimba na ndoa za utotoni pamoja na madhara mengine ya kiafya na kisaikolojia.

Mila hutumika kufanya matambiko na kutii masharti ya mizimu ya baadhi ya jamii zinazoamini kuwa ukeketaji unaondoa mikosi katika familia, pia zipo sababu za kiuchumi ambapo ngariba na wazee wa mila hulipwa fedha au mali kadhaa ili kutimiza azma hiyo.

Kwa upande mwingine, wazazi wa watoto wanaokeketwa huwa na matarajio ya kuwaoza mabinti zao kwa lengo la kupata kipato kupitia mahari na zawadi nyingine zinazotolewa, pia jamii inaamini kuwa waliokeketwa wanaheshimika ndani ya familia zao na katika jamii kwa ujumla.

Jamii zinaamini kuwa ukeketaji ni tiba ya ugonjwa wa ‘Lawalawa’ ambao kitaalamu ni Urinary Track Infection (UTI) ambao ni maambukizi kwenye via vya nje vya uzazi kwa mtoto wa kike au mwanamke.

Ukeketaji una madhara makubwa kwa wanawake na watoto wa kike, ikiwa ni pamoja na athari za kisaikolojia kama msongo wa mawazo kwani vitendo hivyo hufanywa bila ridhaa ya wahusika.

Madhara ya kiafya kama maumivu makali, kutokwa damu nyingi, kuuguza kidonda, changamoto za kujifungua na uwezekano wa kupoteza maisha, huku madhara mengine ya kiafya ni maambukizi ya magonjwa ya ngono, pamoja na maambukizi ya kujirudia UTI.

Wataalamu wanasema ukeketaji unaweza kueneza Virusi vya UKIMWI kutoka kwa ngariba kwenda kwa wateja wao au kwa wasichana nanaokeketwa kwa kuchangia kifaa kimoja, mimba kinzani zinazosababishwa na kovu la ukeketaji unaweza kusababisha tundu kati ya njia ya uzazi na uke au njia ya haja kubwa na uke (fistula) hali ambayo inamwathiri mwanamke kwa kiasi kikubwa.

Kadhalika, mtoto anaweza kupata changamoto wakati wa kujifungua ambazo zinaweza kumsababishia mtindio wa ubongo na mateso katika maisha yake yote.

Serikali inasema katika kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto nchini serikali na wadau wamefanikiwa kuanzishwa kwa Kamati za Ulinzi wa Wanawake na Watoto 18,618 kwenye mikoa, halmashauri, kata hadi ngazi za vijiji na mtaa.

Aidha, nyumba salama tisa zimeanzishwa kwa ajili ya kuwahifadhi na kuwatunza waathirika waliokimbia ukeketaji kwenye mikoa yenye kiwango cha juu cha ukeketaji, kuanzishwa kwa vituo vya mkono kwa mkono 14 kwenye mikoa 10 ya Tanzania Bara na kuanzishwa kwa Dawati la Jinsia na Watoto katika vituo 420 vya Jeshi la Polisi nchini.

Kwa ujumla pamoja na jitihada bado tatizo ni kubwa ni lazima wadau, NGO’s na serikali kuongeza bidii katika kupambana na ukeketaji kwa kuwa mikoa inayotajwa imefanya hivyo kwa muda mrefu.

Ni lazima kubadili muundo wa kupambana na mambo hayo kwa kuwa sheria kali zipo, lakini bado vimeendelea kujitokeza ni muhimu kufanya utafiti wa visababishi na kuwa na mbinu ya kuvikabili.

***Mungu ibariki Tanzania***

















Ilikuwa shangwe na nderemo kwa familia ya Hillary Ndeng'aso na Josephine Mosha. Baada ya kufunda ndoa katika Parokia ya moyo Safi wa Bikira Maria Kikelelwa Rombo, Kilimanjaro, Disemba 29 mwaka jana.





# MITINDO

Na Christina Mwakangale

## HUJAKOSEA KUVAA SATINI

# Mng'aro wake si mchezo

WANAWAKE wanapenda kuvaa nguo zinazotokana na vitambaa vizuri, lakini wengi hawajui namna ya kuchagua na hivyo inakuwa vigumu kwao kupendeza.

Kulingana na historia ya mavazi, wabunifu wanapata tabu kuchagua aina ya vitambaa ambavyo itakuwa rahisi kufuliwa na wakati huo huo kutopoteza asili yake.

Kwa hiyo, mavazi ya satini inachukuliwa kuwa moja ya bidhaa zinazovutia zaidi za kike ambazo ni rahisi kusafishwa na kubaki katika mng'ao wake wa awali.

Nguo hizi zinapendeza zaidi kuvaliwa nyakati za baridi kutokana na uwezo wake wa kuhifadhi joto na kumfanya mvaaji kuona raha zaidi.

Kutokana na aina ya nguo kuwa ya kuteleza, unatakiwa kuwa mwangalifu kidogo.

Mifano ambayo nguo za satini zimekusudiwa kwa ajili ya hafla za jioni, huwa na mvunjiko juu na urefu unaoishia miguuni.

Mtindo wa Low Classic na Nanushka, kwa mfano, ni nzuri kuvaa na suruali.


Nguo kutoka kwa chapa ya Materiel na Lee Mathews, itaonekana kupendeza zaidi kama utavaa na koti zuri, viatu aina ya buti .

Kitu cha kuzingati ni kuepuka kuvaa nguo za Satini katika kipindi cha joto hasa nyakati za mchana, kwani mara nyingi zinageuka kuwa kero na kumfanya mtu kutokuwa na furaha.



UREMBO

Na Mary Geofrey



# MIGUU, MIKONO MURUA

## Njia hizi zitaondoa sugu kwenye viwiko

NGOZI nyeusi katika magoti na nyuma ya mikono hutokana na mkusanyiko wa seli zilizokufa.

Pia misuguano ya mikono na vitu mbalimbali inachangia kuweka alama hiyo, kama meza na viti vya ofisini huchangia hali hiyo.

Kama una magoti na viwiko vyenye rangi nyeusi tumia njia hizi asili ili kuweza kuondoa.

**Juisi ya Aloe Vera**

Juice ya Aloe Vera inasaidia kuondoa weusi, unachotakiwa ni kupaka juice hiyo kwenye sehemu yenye weusi na uache kwa nusu saa kisha nawa na upake mafuta. Rudia kufanya hivi mara mbili kila siku.

**Binzari Manjano, Asali na Maziwa.**

Changanya vyote hivi utapata mchanganyiko mzito, paka kwenye magoti na kwenye mikono yako palipo na weusi. Kaa nayo kwa dakika 30, nawa na paka moisturizer. Rudia hii kila siku kwa wiki tatu hadi nne, utapata matokeo mazuri.

**Ndimu.**

Chukua pamba na uitumie kupaka juice ya ndimu katika sehemu zenye weusi. Au unaweza kuikata tu ndimu na kuipaka moja kwa moja kwenye sehemu zenye weusi. Kaa nayo kwa saa moja kisha nawa.

Rudia hivi kila siku hadi weusi utakapopotea.

**Tumia mafuta ya mzaituni na Sukari**

Changanya vizuri, hii itakuwa kama exfoliation/scrub kwa ajili ya magoti na mikono.

Paka katika hizo sehemu zenye weusi kisha kuwa kama una-massage polepole, nawa kwa maji ya uvuguvugu kisha paka moisturizer.

MAPISHI

Na Mary Geofrey

# Namna Kuku anavyopikwa

KUKU ana namna mbalimbali ya kumpika na ukafurahia mlo wako.

Leo katika safu hii tutaelekezana namna ya kupika kuku awe mlaini, mwenye ladha na anayevutia kwa wanaomtizama.

Mapishi haya ya kuku yanakupa nafasi ya kuona ubora wa mapishi kwa mlo wa muda wowote unaopendelea.

Unaweza kula chakula hiki asubuhi, mchana au jioni.

Mahitaji

Kuku nusu kilo , asali vijiko vinne, sukari ya brown kijiko kimoja na nusu na soya sauce nusu kikombe.

Mahitaji mengine ni tangawizi vijiko viwili vya chai, kitunguu saumu vijiko viwili vya chai, chilli sauce vijiko vitatu vya mezani, chumvi kiasi na Cayenne pepper kiasi.

Kadhalika utahitaji mafuta ya mzaituni vijiko vitano vya chakula, Currypowder kijiko kimoja cha chai, coriander powder kijiko kimoja cha chai na ndimu moja.

Namna ya kutengeneza

Mapishi hayo ya kuku yanakupa nafasi ya kuona ubora wa mapishi kwa mlo wa muda wowote unaopendelea.

Unaweza kula chakula hiki asubuhi, mchana au jioni. Ndio ubora wa kuku aliyepikwa kwa staili hii.

Changanya pamoja sukari, asali, soy sauce, tangawizi, kitunguu saumu na chilli sauce kwenye kibakuli kidogo.

Safisha kuku, mkaushe maji, mkate vipande vidogo vidogo muweke kwenye kikaangio, mnyunyizie chumvi, cayenne pepper na ndimu kiasi.

Weka mafuta jikoni kisha weka kuku na anza kumgeuza geuza kuku mpaka mafuta yapate moto, usiache kugeuza mpaka kuku awe wa brown.

Weka viungo vilivyobaki currypowder na coriander powder, koroga kwa dakika tano.

Mwisho mwagia sauce uliyoandaa, usifunike. Pika hadi sauce iwe nzito.



MAISHA NI NYUMBA

**Na Elizabeth Zaya**



# Hivi ndivyo unapaswa kusafisha sofa

WASWAHILI husema umaridadi huficha umaskini. Huu ni msemo mzuri kwa kutamkwa lakini pia unatafakarisha.

Leo,nataka tuangalie umaridadi katika usafi wa sofa kwa sababu hili nalo ni kiungo muhimu cha kung`arisha na kuleta mvuto ndani ya nyumba. Hili pia ni kama ilivyo katika usafi wa mambo mengine katika nyumba, hivyo linahitaji usafi tena kwa umaridadi wa hali ya juu, hususani kwa nyumba zenye familia kubwa.

Baadhi huwa hatuna utaratibu wa kusafisha sofa zetu mara kwa mara kwa sababu huenda ni kutokujua kwamba zinatakiwa kusafishwa au kutokujua vitu vinavyotumika katika kusafishia na mahali pa kuvipata.

Sofa zikifutwa kawaida au kwa kutumia maji matokeo yake huwa si mazuri kwa kuwa badala ya kung`ara, huanza kuchafuka na kuchakaa zaidi.

Kwa wale wanaomiliki sofa za vitambaa, wanatakiwa kutumia njia sahihi zaidi ya kusafisha badala ya kufuta kienyeji ili kuzitunza zisiharibike kwa sababu kitambaa ndicho kiko katika hatari zaidi ya kuharibika endapo utaratibu mzuri hautafuatwa wakati wa kusafisha.

Yako maji maalumu au kwa lugha nyingine 'spray' inayotumika kusafishia sofa hizo, hivyo ni vyema ukaitafuta kwa sababu inapatikana kwa wingi madukani.

Lakini kabla ya kuanza kutumia, hakikisha sofa zako zimepanguswa na kutolewa vumbi lililokuwa limeng`ang`ania kwa kutumia kifaa maalumu cha kupuliza vumbi au kwa kutumia kitambaa kisafi. Baada ya kuhakikisha umesafisha kila kona, ndipo unatakiwa kuanza kuipulizia.

Kwa kuzingatia ujazo katika chupa hizo maalumu za maji ya kusafishia sofa, unaweza kutambua utumie chupa ngapi na kwa sofa ngapi hasa kulingana na ukubwa wa tatizo japokuwa naamini moja inaweza kutosha labda kama imechafuka kupitiliza.

Unachopaswa kufanya ni kupulizia katika sehemu ndogondogo ili wakati huo huo uwe unafuta na kitambaa kisafi, na unatakiwa kufanya hivyo mpaka umalize.

Baada ya kumaliza kazi hiyo katika maeneo yote unaweza kuliacha likauke na hapo ndipo utaanza kuona matokeo mazuri kwa sababu mng'ao wa rangi yake utakuwa mzuri zaidi.

Kumbuka kwamba kufanya usafi huo katika sofa lako hauhitaji gharama kubwa sana endapo utafanya mwenyewe, isipokuwa uamue kutumia gharama kubwa kwa matakwa yako kwa kutumia wataalamu wa kukodi.

Pia kadri utakavyojenga utaratibu wa kupenda kusafisha sofa lako mara kwa mara ndivyo hivyo gharama itazidi kuwa ndogo kwa sababu hutatumia 'spray' nyingi kama ambavyo utasafisha zikiwa zimechafuka sana.



## Namna ya kuweka mapazia ya ndoano




UWEKAJI wa mapazia kwenye madirisha ya nyumba ni mtindo wa kale lakini kila kukicha unazidi kuboreshwa na kuwa pambo muhimu katika kupendezesha nyumba. Katika miaka ya hivi karibuni mtindo wa kuweka mapazia marefu katika stendi ya plastiki imekuwa jambo la kawaida na hivyo watu wengi huvutika nao.

Kutokana na umuhimu wake nakupa dondoo za namna ya kupachika pazia katika stendi yake.

1: Kwanza weka ndoano kwenye mapazia, ili iwe rahisi kupachika katika bomba la plastiki.
2: Tundika mapazia kwenye mabomba ya plastiki yaliyowekwa katika stendi yake.
3: Chagua rangi inayoendana kati ya pazia na mabomba ili kuongeza mvuto wa nyumba.
4: Hakikisha mapazia yanakuwa sawa kwa ukubwa ili mwonekano wake uwe mzuri.

# KATUNI



KATUNIKA KI'DOMOKRASIA
BY ABDUL KINGO - 2022
SMS - 0621 412 879
JUKWAANI
MAISHA
SISI
UNATAKA TUACHANE KWANI USHA-MALIZA KIINUA MGONGO?
EMBU NIACHE NIFE KWA HESHIMA UNADHANI KUFIA GESTI SIFA NZURI KWA MSTAAFU?
DALADALA ZA USIKU MWINGI...
UMELEWA UNATUFOKEA KWA MAKELELE KAA KIMYA!
NYIE MNANIONEA GERE MIMI KUNYWA BIA!
ANARUSHA MATE BALAA
ALAFU ANA MAPENGO
BASI LENYEWE HALINA MZIKI NIACHENI MIE NIJIMWAGEEE
KONDA MJINGA DEREVA BWEGE TRANS
DUH! KAZI IMEKUWA NGUMU!
UHAME USHAPEWA NOTISI
MBONA NA YEYE MLEVI?
SAA NGAPI JANA
KAWAULIZE KITUONI WAMENIACHIA SAA NGAPI TOKA SERO? SIKUWA KWA VERO
MAPENZI YETU USI-YAINGILIE
NAKUONA KONTAWA UKWENI ETI 'MUHASIBU'
MUHASIBU SIO KUHESABU HELA TU, HATA KUHE-SABU MITAA...
*KINYUNYIZO CHA LEO...
NENDA MBELE, GEUKA NA NYUMA...

# Viongozi Afrika kukutana

**ADDIS ABABA,** ETHIOPIA

VIONGOZI wa Mataifa ya Afrika, wameanza mkutano wao ambao unafanyika chini ya kiwingu cha wimbi jipya la mapinduzi ya kijeshi barani humo na mapambano dhidi ya corona.

Pamoja na masuala hayo mawili mkutano huo, pia unalenga kutafuta uungwaji mkono wa kushinikiza bara la Afrika kupata uwakilishi ndani ya Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa.

Katika taarifa yake kuelekea mkutano huo, shirika la kimataifa la masuala ya mizozo limesema suala la usitishaji mapigano nchini Ethiopia, kuunga mkono mazungumzo kwenye mzozo wa kanda ya Sahel na kuufanyia mageuzi ujumbe wa kijeshi nchini Somalia vinapaswa kuwa vipaumbele katika mkutano huo.

Umoja wa Afrika ambao mwezi Julai utatimiza miaka 20 tangu kuundwa kwake, umekuwa ukikosolewa kwa kushindwa kushughulikia mizozo inayozuilika kila wakati ndani ya bara hilo lenye wakazi bilioni 1.3.



Wanajeshi wa Ukraine wakiwa katika uwanja wa mazoezi, Feruari 03, 2022. **PICHA: DW**

# Macron, Scholz kufanya ziara Urusi

**PARIS,** UFARANSA

RAIS Emmanuel Macron wa Ufaransa na Kansela Olaf Scolz wa Ujerumani, watafanya ziara nchini Urusi na Ukraine kwa nyakati tofauti katika siku chache zinazokuja.

Ziara hizo ni sehemu ya juhudi za kidiplomasia za kuizuia Urusi kuivamia Ukraine.

Rais Macron atakwenda Urusi siku ya Jumatatu na baadae mjini Kyiv siku inayofuata kuongeza msukumo wa kufanyika majadiliano na Rais Vladimir Putin ili kupunguza wasiwasi wa kutokea mzozo kamili wa kijeshi.

Kwa upande wake, Kansela Scholz ambaye serikali yake inahimiza njia za kidiplomaisa katika mzozo huo na Urusi, atafanya ziara nchini Ukraine Februari 14 na kisha kesho yake atakwenda Urusi kwa lengo la kufanya mazungumzo ya kina na viongozi wa pande hizo mbili.

Jana mawaziri wa mambo ya kigeni wa Marekani na Ukraine walizungumza kwa njia ya simu kujadili namna ya kuishinikiza Urusi kuridhia majadiliano na kupunguza kitisho cha usalama kwenye mpaka na Ukraine.

# Onyo wakati kimbunga Batsirai kinakaribia kuipiga Madagascar

**NEWYORK,** MAREKANI

Umoja wa Mataifa umeonya kwamba kimbunga Batsirai kinachoelekea nchini Madagascar, kinaweza kuwaathiri takribani watu 600,000. Kimbunga hicho kinatarajiwa kutua katika pwani ya mashariki ya kisiwa hicho leo, baada ya kupita nchini Mauritius.

Batsirai kinakuja wiki moja baada ya dhoruba ya kitropiki ya Ana kusababisha madhara katika eneo hilo.

Umoja huo umesema ndege za uokozi na boti zimewekwa tayari na maandalizi yamefanyika kwa ajili ya ugavi wa mahitaji ya kibinadamu.

Kimbunga Ana kiliua zaidi ya watu 50, na wengine 70,000 walipoteza makazi yao.

Umesema watu wengi wanakabiliwa na hatari ya kukumbwa tena na kimbunga Batsirai.

Shirika la misaada la Msalaba Mwekundu, pia limetoa tahadhari kwamba dhoruba hiyo mpya huenda ikauongeza makali ya njaa unaoikabili nchi hiyo.

# Waasi wa Darfur bado wapo Libya

WATAALAMU wa Umoja wa Mataifa wamesema makundi ya waasi kutoka jimbo la Darfur, ambayo yalitia saini mkataba wa amani na serikali ya Sudan mwaka 2020, bado yanaendelea na operesheni zake nchini Libya.

Katika ripoti yake kwa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ilisema vyanzo kadhaa kutoka mtandao wa makundi hayo vimefahamisha kuwa hawana mpango wa kuondoka Libya kwa sababu wanapata fedha nyingi, chakula na hata mafuta.

Kamanda mmoja wa makundi hayo, alinukuliwa katika ripoti hiyo akisema wataendelea kufanya operesheni zao katika jimbo la Darfur nchini Sudan na Benghazi nchini Libya.

Kuendelea kuwepo kwa makundi hayo ni kinyume cha makubaliano ya kusitisha vita ya mwaka 2020 yaliyotaka makundi hayo na mengine kuondoka nchini Libya ili kuipatia nafasi nchi hiyo kurejesha uthabiti.

# Ujerumani yajiondoa kutoa silaha

**BERLIN,** UJERUMANI

WASHIRIKA wa NATO, Marekani, Uingereza na mataifa ya Baltic yametuma silaha nchini Ukraine. Hata hivyo, Ujerumani imeweka wazi kwamba haitofuata mkondo huo.

Mpaka sasa, Berlin imetoa kofia 5,000 za kujihami na ilisema inapendelea suluhisho la kidiplomasia.

Serikali ya Ujerumani, inayoundwa na chama cha siasa za mrengo wa kati-kushoto cha (SPD), chama cha watetezi wa mazingira cha die Grüne, na kile kinachoegemea biashara cha Free Democrats (FDP), kina sera kali ya uuzaji wa silaha ambayo hairuhusu kuuza silaha katika maeneo yenye mizozo.

Sera sawa na hiyo ilikuwepo chini ya muungano uliopita ulioongozwa na Angela Merkel. Lakini pamoja na hayo, mwaka 2021 ilishuhudia rekodi ya mauzo ya silaha zenye thamani ya euro bilioni 9.35, sawa na dola bilioni 10.65.

Lakini kumekuwa na miito ya kupitia upya sera ya mauzo ya silaha za Ujerumani.

"Tufungue mjadala juu ya iwapo Ujerumani inapaswa kubadili msimamo huu," Viola von Cramon, mbunge wa bunge la Ulaya kutoka chama cha Kijani na makamu mwenyekiti wa ujumbe wa bunge hilo nchini Ukraine, aliiambia DW.

Alisema pia Ujerumani inapaswa kuchukuwa msimamo mkali zaidi kuelekea Urusi, na kuelezea wasiwasi kuhusu pendekezo la Uturuki kuwa mpatanishi kati ya nchi hizo mbili.

MAKALA

# LEO FEDHA IMEZIDI UTU WA BINADAMU KATIKA JAMII



Na Magabilo Masambu

LAKINI ufahamu neno hili ya kuwa, siku za mwisho kutakuwako nyakati za hatari. Maana watu watakuwa kwenye kujipenda wenyewe, wenye kupenda fedha, wenye kujisifu, wenye kiburi, wenye kutukana, wasiotii wazazi wao, wasio na shukrani, wasio safi, wasiowapenda wa kwao, wasiotaka kufanya suluhu, wasingiziaji, wasiojizuia, wakali, wasiopenda mema, wasaliti, wakaidi, wenye kujivuna, wapendao anasa kuliko kumpenda Mungu" ( 2 timotheo 3:1-4)

Siku za hivi karibuni na mpaka sasa tumeendelea kusikia matukio ya Watanzania kuuwana, huku zikitajwa sababu mbalimbali.

Baadhi ya sababu hizo zimeelezwa kuwa ni kutokana na wivu wa mapenzi, imani za kishirikina na migogoro ya ardhi.

Lakini wako pia ambao wametuhumiwa kuwaua wazazi wao wa kuwazaa. Tumesikia mambo haya yakitokea Arusha, Kilimanjaro, Mbeya na kwingineko.

Mahali pengine tukasikia habari ya mama kuwanywesha sumu watoto wake na yeye kunywa bahati tu akanusurika sababu inayotajwa ni ugumu wa maisha. Aliona asingeweza kuwahudumia, hivyo akaona ni bora afe nao. Haya ni mambo ambayo yanatutaka kama Watanzania kwa ujumla bila kujali tofauti zetu zozote, kuyatafakari kwa kina kuona namna bora ya kuyapunguza kama si kuyamaliza.

Nimenukuu hapo juu maandiko matakatifu yanavyoeleza kuelekea siku za mwisho japo yanasema pia kuwa myaonapo haya ni utungu tu ingali mwisho bado.

Pamoja na kwamba zinasemwa sababu kadhaa ambazo baadhi nimezitaja hapo awali, nafikiri sababu zote hizo zaweza kuwa za pili na tusipotafuta kiini hasa, mambo haya yatamkuta kila mmoja wetu. Leo tunayaona kwa wenzetu kesho tutayaona majumbani mwetu.

"Lakini ni dhahiri kwamba tumefanya makosa katika kuchagua silaha, kwani silaha tuliyochagua ni fedha.

Tunataka kuondoa unyonge wetu kwa kutumia silaha ya wenye nguvu, silaha ambayo sisi wenyewe hatuna. Katika mazungumzo yetu na mawazo yetu na vitendo vyetu ni kama tumekata shauri kwamba bila fedha mapinduzi yetu hayawezekani. Ni kama tumesema fedha ndiyo msingi wa maendeleo na kwamba bila fedha hakuna maendeleo.

Hii ndiyo imani yetu ya sasa. Viongozi wa TANU, wa serikali, wanasiasa, watumishi na wananchi wote mawazo na matumaini yao ni kwenye fedha. Ni kama wote tumekubaliana na tukasema kwa sauti moja kwamba tukipata fedha tutaendelea, bila fedha hatutaendelea! ( Mwalimu JK Nyerere, Azimio la Arusha 1967, UK 9)"

Kwa maoni yangu, matatizo tunayoyaona haya leo ni matokeo ya kudhani kwamba fedha ni kila kitu na kwamba ndio msingi wa maendeleo. Lakini mtazamo wa Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, aliamini kwamba fedha ni matokeo ya kazi ikiwa na maana kwamba ukifanya kazi ukazalisha utapata fedha. Ni kweli kwamba pengine ili kufanya kazi na uzalishe unahitaji fedha (mtaji).

Kundi mmoja lisilo na ajira linaweza kutumia sababu ya kukosa fedha kama mtaji ili kuzalisha lakini vipi kundi la pili lenye kazi tayari linafanya nini kuzalisha kwa wingi na kwa ubora ili lipate fedha nyingi zaidi kama matokeo ya kazi zao?

Kama upo kiwandani unazalisha bidhaa zenye ubora kiasi gani ili kushindana katika soko, kama una shamba unawezaje kulitumia kuzalisha chakula na ziada kila mmoja anajua anafanya nini.

Nadhani haya matukio tunayoyaona leo watu wakiuana, ukiyafuatilia kwa karibu sana pamoja na sababu zinazotajwa na nyinginezo kama za kimaadili na malezi, utagundua tatizo kubwa ni watu kupenda fedha zaidi kuliko utu wa watu wengine. Mtu yuko tayari kufanya lolote ili apate fedha, hajalishi anamuua nani ndiyo maana tumesikia mpaka habari za watoto kuwaua wazazi wao.

Sababu za yule wa Kilimanjaro zinatajwa ni mafao ya mama yake, yule wa Njiro Arusha ni juu ya mali za mama yake, yule wa Mbeya ni imani za kishirikina lakini pia akidai kwamba baba yake alikuwa anafanya asifanikiwe. Tuhuma za askari polisi Mtwara kumuua mfanyabiashara wa madini ni fedha ilikuwa inatafutwa. Hiyo ni mifano michache tu inayoonyesha mawazo yetu ni juu ya fedha na mafanikio.

Leo hata mahubiri katika baadhi ya makanisa, sijajua misikitini, tutakuwa mashahidi kwamba kinachohubiriwa zaidi ni mafanikio ya kifedha kuliko neno la Mungu.

Rudi kwenye familia zetu leo hata undugu wetu umeunganishwa na fedha. Mtu unaonekana wa maana kama unatoa fedha zaidi. Mwenye fedha ndiye anayesikilizwa hata akiwa na umri mdogo, ndiye anayekuwa mwenyekiti wa vikao vya ukoo ingawa kuna watu wazima.

Upendo miongoni mwetu umetoweka badala yake unyama umetamalaki. Ukarimu pia umeondoka hata matajiri ambao wangaliweza kuandaa sherehe za harusi kwa kutumia fedha walizonazo kama ilivyokuwa zamani mtu anaandaa shughuli na kuwakaribisha ndugu jamaa na marafiki wajumuike, wanawachangisha hata masikini ili kushiriki. Fedha imekuwa na nguvu kuliko utu. Ni kweli kwamba inawezekana zisipatikane njia sahihi za kumaliza tatizo hili lakini tunaweza kujaribu kulipunguza.

Moja, ni muhimu serikali kufikiria namna ya kuboresha maisha ya watu zaidi na eneo moja kubwa ni sekta ya kilimo ili watu wawe na chakula cha kutosha. Watu wakishakuwa na chakula kingi, mahitaji ya fedha yatapungua. Kinachotakiwa kufanyika kwenye kilimo ni kupunguza gharama za pembejeo ili watu walime kwa urahisi, lakini pia tuwe na mifumo ya umwagiliaji katika baadhi ya maeneo ya nchi kunakokubali mazao ili hayo maeneo yalishe nchi nzima.

Ni aibu sana kwa nchi iliyojaa mapori ya mashamba, mito na maziwa leo gunia la mahindi linafika Sh. 100,000.

Wizara ya Kilimo inapaswa kujitafakari katika hili, kilimo cha kutegemea mvua kimepitwa na wakati badala yake wananchi wahamasishwe na kuwekewa miundombinu ya kumwagilia ili wazalishe chakula cha kutosha na kurudisha ukaribu na upendo kwenye familia zao. Kwa sasa watu wanashindwa kuishi na ndugu kwenye familia kutokana na kutokuwa na chakula cha kutosha na mahitaji mengine ya msingi.

Pili, kama jamii tuimarishe misingi ya malezi. Kwa sasa hatulei watoto badala yake tunawakuza kwa kuwapa chakula na mavazi pekee.

Mtoto anayekulia shuleni hawezi kamwe kuwa na mapenzi na wazazi. Zamani mtoto alikuwa wa jamii leo watoto ni wetu wazazi na akimtukana mzee wa jirani, hatuna habari, tunafurahia lakini baada ya muda hao hao ndio wanaotuuwa.

Tatu, tujitahidi kutafuta mali na fedha za halali. Tuishi maisha yetu tusipende na kutamani maisha ya wengine. Mwenyezi Mungu anatupatia wote, ni wakati tu unakuwa haujafika kwa maana kuna majira ya huzuni na furaha.

Kama unapitia magumu leo, kesho utakuwa mwenye furaha. Ni suala la kuwa na subira kwa sababu ugumu wa maisha ulio nao hautakuwa wa kudumu. Fedha si kila kitu katika maisha pamoja na kwamba tunazihitaji kupata mahitaji yetu ya kila siku.

**0689157789**
**magabilomjalifu@gmail.com**
**ARUSHA-TANZANIA**

BURUDANI ILIYOTIKISA ENZI HIZO

# Utata wa mtunzi wa wimbo 'Malaika'



Na Adam Fungamwango

MALAIKA, nakupenda Malaika. Nami nifanyeje, kijana mwenzio, nashindwa na mali sina weee, ningekuoa Malaika, Kidege, hukuwaza kidege. Ningekuoa aaa mama, ningekuoa aaa dada, nashindwa na mali sina wee, ningekuoa Malaika. Pesa zasumbua roho yangu, nami nifanyeje, kijana mwenzio, nashindwa na mali sina wee, ningekuoa Malaika."

NI zaidi ya miaka 70 sasa tangu utungwe na kurekodiwa lakini hadi leo umekuwa moja ya nyimbo bora kabisa duniani zinazoendelea kuishi na kuzidi kupendwa kizazi hadi kizazi.

Huwezi kwenda kwenye bendi yoyote ile inayopiga 'laivu' duniani bila wimbo huo kupigwa, kwa kuimbwa au vyombo vitupu. Sababu kubwa ni kwamba umekuwa wimbo mkubwa mno duniani lakini kuna utata mkubwa kuhusu mtunzi halisi wa wimbo huo.

Waandishi, wafuatiliaji wa masuala ya muziki na watafiti, walifanya uchunguzi huku na huko kujua ni nani hasa mtunzi halisi wa wimbo huo.

Awali kabisa ni wimbo ambao umerekodiwa na bendi nyingi sana duniani kuanzia kundi maarufu la Boney M lililovuma sana miaka ya 1970, lenye makazi yake nchini Ujerumani, Miriam Makeba na Harry Belafonte, Angelique Kidjo, Pete Seeger na wanamuziki wengi sana duniani, waliurekodi wimbo huu wakiimba kwa lugha hiyo hiyo ya Kiswahili lakini kila mmoja kwa staili yake, na mtindo wake wa muziki walioamua kupiga.

Mtu aliyenufaika sana na wimbo huu, kwa kulipwa mirahaba na makundi yote yaliyotaka kupiga kuonana naye na kumlipa kwanza ni Fadhili William. Huyu ni mwanamuziki maarufu sana wa Kenya aliyezaliwa mwaka 1938 na kufariki dunia Februari 11, 2001.

Ingawa alitunga, kupiga na kurekodi nyimbo nyingi kama 'Taxi Driver', 'Ewe Wangu', 'Naenda Safari' na zingine nyingi lakini wimbo uliomfaidisha na kumpa maisha mazuri ni 'Malaika' aliourekodi mwaka 1963 na bendi yake ya Jambo Boys.

Yeye ndiye aliyeusajili kama mtunzi halisi na aliyekuwa na hakimiliki ya wimbo huo. Ni wimbo uliompa pesa nyingi sana kwa bendi nyingi kutaka kuurekodi, hadi alipofariki dunia.

Hata hivyo, wachunguzi wa masuala ya muziki waligundua utata mwingine. Wakatajwa watunzi wengine kuwa ni Lucas Tututu wa Mombasa lakini pia Andrea Sholo naye akatajwa kuwa mtunzi. Baadaye, ikaja kugundulika kuwa mtunzi halisi ni mtu mmoja Mtanzania, anayeitwa Adam Salim. Wachunguzi wengi, waandishi wa habari na wadau wa muziki, mwisho wao walifikia hapo na wakakubaliana hivyo.

Mtanzania huyu mwenyeji wa Moshi mkoani Kilimanjaro aliyezaliwa mwaka 1926, ndiye aliyeutunga wimbo huo. Ndiye mtunzi halisi wa wimbo huo lakini hakupata chochote zaidi ya Sh. 60 alizolipwa alipokwenda kuurekodi na kuuza kwenye kampuni ya kurekodia Columbia East African Music mwaka 1950.

Ingawa kwa wakati huo zilikuwa nyingi, hapo ilikuwa ndiyo mwisho wa kupata pesa zingine kwani baadaye ilikuwa kama ameuuza. Sijui nini kilitokea, wimbo huo baadaye ukaja kuchukuliwa na Fadhili William kuwa ndiye mtunzi na aliyefaidika kwa mirabaha kutoka pande zote za dunia.

Uchunguzi wao wote hao ukagundua kuwa mtunzi wa wimbo huo, Adam alimtungia mpenzi wake aliyeitwa Halima Ramadhani Maruwa aliyekuwa akiishi Kenya. Mbongo huyo akiwa nchini Kenya, alikuwa akifanya kazi ya umakenika au siku hizi wanaita fundi gereji. Lakini pia ni mwanamuziki aliyekuwa na bendi yake akiita Adam & Trio iliyokuwa ikipiga muziki kila wiki kwenye mahoteli na baa mbalimbali.

Hata hivyo wazazi wa Halima hawakumpenda Adam, licha ya binti mwenyewe kulalamika sana, lakini haikusaidia. Kuwa mwanamuziki pia kulichangia sana wazazi hao kukataa binti yao asiolewe naye.

Kwanza wazazi wa msichana huyo walikuwa itikadi na imani yao haiendani na muziki, halafu mara nyingi kuna dhana kuwa wanamuziki ni watu wasiotulia, wahuni, hivyo binti yao anaweza kutopata matunzo mazuri, akateseka. Kisa hiki kilimalizika kwa binti huyo kuolewa na mwanaume mmoja tajiri kwenye asili ya kiasia.

Hilo lilimuumiza sana Mtanzania huyo, ndipo akautunga wimbo huo kama inavyojieleza kuwa anampenda sana, lakini afanye nini, mali hana, kama angekuwa na pesa angemuoa malaika huyo.

Kuna wengine wanasema kuwa Adam alimwandikia barua ya huzuni mpenzi wake Halima na baadhi ya maneno yaliyokuwa kwenye barua hiyo ndiyo aliyachukua na kuyafanya mashairi ya wimbo huo.

Kwa uchache hicho ndicho kisa cha wimbo wa 'Malaika' uliotungwa na Mtanzania Adam na kumnufaisha Mkenya Fadhili.

Mtanzania huyo alitunga kwa huzuni ya kunyimwa mpenzi wake aliyeolewa na tajiri huyo. Alifanya hivyo ili tu kutoa la moyoni mwake badala ya kukaa nalo rohoni.

Akaufanya wimbo akaurekodi bila kujua kuwa utakuwa wimbo mkubwa sana duniani. Bahati mbaya sana kama alivyotakaliwa na wazazi wa binti na kutoishi naye kwa muda mrefu, pia hakunufaika sana na wimbo wa 'Malaika.'

**Tuma meseji 0716 350534**

# HADITHI

TINA, msichana kutoka Mpanda, mkoani Katavi anafiwa na wazazi wake wote wawili kwa ajali ya gari akiwa na miaka 10 tu. Tabu alizozipata kutokana na kunyanyaswa na ndugu zake, zilimfanya kuishi maisha ya mateso. Hata shule aliishia la saba tu. Alipofikisha umri wa miaka 18 akakimbilia Dar es Salaam na kuanza kufanya kazi za ndani. Baadaye akabahatika kupata kazi za ndani kwa mfanyabiashara mmoja maarufu, Hafidh Chilambo. Mfanyabiashara huyo anafariki kwa kula chakula kilichowekwa sumu. Chakula hicho kilipikwa na Tina. Mahakama Kuu inamhukumu adhabu ya kunyongwa hadi kufa. Je ni wafanyabiashara wenzake Chilambo ndiyo waliomtuma msichana huyo kwa kumwahidi mamilioni ya pesa kutokana na ugomvi wa kibiashara? Au ni kwa sababu hajalipwa mshahara wake wa miezi sita aliokuwa anadai? Fuatilia kila nakala ya Nipashe ili kuupata ukweli ulio nyuma ya pazia wa sakata hili.

# Ajenda ya Siri-16

**Na Adam Fungamwango**
**(0716 350534)**

ALICHUKUA tena simu yake na kumpigia rafiki yake Wakili Florence Tinga.

"Niambie Eddy."

"Poa tu, mambo vipi?

"Safi, umenipigia asubuhi hii nadhani kutakuwa na jambo."

"Jambo lipo, ila tukutane ofisini kwangu saa sita mchana leo."

"Vipi, hebu nipe muhtasari Eddy ni jambo gani hilo?"

"Nina mzigo wako."

"Nadhani itakuwa ni ile ya yule msichana, ndiyo?"

"Uko sahihi."

"Umekamilisha kila kitu?"

"Siwezi kusema kila kitu, ila nadhani kuna vitu ambavyo vitatusaidia."

"Okay, nakuja."

Wakati huo alimwita Tinga akijua kesho yake ana kibarua kingine cha kwenda kwenye hoteli ya Moonlight, Sinza Dar es Salaam. Ilikuwa moja kati ya maeneo ambayo alitakiwa kwenda kukamilisha uchunguzi kwani baada ya kuwahoji wote wawili, Mzee Kalango na Hussein, aliona upelelezi wake hautatimia mpaka afike kwenye hoteli hiyo.

**************************************

Mvua kubwa Dar es Salaam ilisababisha sehemu zingine za barabara kutopitika kwa urahisi. Japo kuna maeneo ambayo kiasi kikubwa barabara imetengenezwa na kuwekwa lami safi tofauti na miaka ya nyuma, kwa sababu ujenzi bado unaendelea, ziko sehemu ambazo bado hazijakamilka. Ndizo zinazoleta usumbufu mkubwa kwa madereva pamoja na watembea kwa miguu.

Kama kawaida alikuwa kwenye gari lake alilolipenda sana kutumia, Nissan Ariya lenye rangi nyeusi. Alilipita daraja la Manzese Uzuri, akitokea maeneo ya Sinza Kijiweni akielekea Tandale.

Alipofika Kwa Mtogole, alikata kulia kwenye barabara isiyo na lami, akaendesha taratibu hadi kufikia sehemu fulani ambayo aliikumbuka. Akapaki Saa ya kwenye gari ilimwonyesha kuwa ni saa kumi na robo jioni. Ndipo alipogundua kuwa kazi aliyotoka kuifanya, alitumia muda wa saa tatu.

Kabla ya kufika pale alikuwa ametoka maeneo ya Sinza Legho kwenye hoteli moja inaitwa Moonlight kama alivyoahidi jana. Huko aliendelea na uchunguzi wake. Alichukua vitu kadhaa ambavyo alidhani vitamsaidia kwenye ushahidi.




**Alitembea kwa taratibu na tahadhari, huku akirudisha kumbukumbu nyuma kwani alishawahi kupita hapo kiasi cha miezi kadhaa iliyopita. Alifika kwenye nyumba aliyoikusudia. Alikuta kinamama wawili wakiwa nje wanasukana.**

Alifika huko kutokana na maelezo aliyoyapata kutoka kwa Mzee Kalango na Hussein.

Ni jana yake alikuwa amekutana na Wakili Tinga ofisini kwake. Kikubwa ilikuwa kumkabidhi nyaraka ambazo zingesaidia kwenye ushahidi wa msichana Tina. Alimkabidhi nakala za nyaraka mbalimbali za karatasi na sauti ambazo zingesaidia, ili kama kuna watu wengine wanahusika na kesi hiyo, basi nao waunganishwe na si msichana huyo peke yake, kwani mwanzo hakukubali kuwa anaweza kuwa yeye peke ndiye aliyepanga njama hizo.

Ambacho wanadhani ni kwamba Tina amefanya mauaji hayo kwa kuahidiwa malipo, ambayo amepewa, amepunjwa au hajapewa kabisa, au ametumiwa na watu wengine kufanya hivyo bila yeye kujua.

"Kwa hiyo bwana Tinga cha kufanya hapo ni nini wewe kama wakili?" Eddy aliuliza.

"Hapa ni kukata rufani ili kesi hii iangaliwe upya. Kama itaonekana Tina bado ana makosa, basi aendelee na adhabu yake, kama kuna watu wengine wanahusika basi nao waunganishwe na mzigo usiwe kwake peke yake, au lolote litakalokuwa baada ya kesi hiyo kupitiwa upya." Tinga alimwambia Eddy.

"Okay, sasa kazi hii utaifanya lini?"

"Nipe wiki moja, nipitie hizi nyaraka ulizonipa na nakala za sauti nizisikilize, halafu nitajua pa kuanzia."

"Okay, nadhani tunaweza kufanikiwa."

"Inawezekana, ila chochote kinaweza kutokea."

Alishuka ndani ya gari na kuanza kutembea taratibu akikwepa matope ya hapa na pale. Kuna sehemu ningine ilibidi kukanyaga mawe katikati ya madimbwi ya maji machafu na matope yaliyowekwa na majirani hapo ili apate nafasi ya kupita.

Alitembea kwa taratibu na tahadhari, huku akirudisha kumbukumbu nyuma kwani alishawahi kupita hapo kiasi cha miezi kadhaa iliyopita.

Alifika kwenye nyumba aliyoikusudia. Alikuta kinamama wawili wakiwa nje wanasukana.

"Habari zenu kinamama." Alisalimia.

"Nzuri baba karibu." Aliitikia mmoja. "Karibu, karibu, shikamoo." Mwingine aliyekuwa anasukwa aliitikia. Ile itikia yake ilimjulisha Eddy kuwa ni mtu ambaye anayemfahamu au amemkumbuka. Aliyekuwa anamsuka mwenzake, mama mtu mzima kidogo alibaki anamshangaa, kwani hajawahi kumwona.

"Karibu ndani." Aliinuka na hapo ndipo alipomwangalia kwa makini. Na yeye akaanza kumkumbuka.

"Wewe ni Mwasi eee."

"Ndiyo karibu." Mwasi alijibu huku akitabasamu, kwani alijua huenda mgeni huyo amemsahau.

"Yupo ndani, twende tu mgeni."

"Mama yupo?"

"Eee yupo."

Aliingia na varandani. Kama kawaida ya nyumba za uswahilini. Zinakuwa na varanda ndefu, halafu pembeni kunakuwa na vyumba.

Wakati huo, Mwasi alikuwa ametangulia mbele na kukata kona kushoto, huku akiita "Mama, mama kuna mgeni."

Aliyetoka kwenye hicho chumba sasa hakuwa Mwasi. Ni bi Mtupeni. "Karibu karibu mwanangu yoyooo, baba huyooo."

"Ahsante mama za siku nyingi."

"Nzuri tu baba, leo naona umetukumbuka. Siamini macho yangu, karibu humu ndani." Aliinginzwa kwenye chumba kingine ambacho kilikuwa na makochi na TV tu basi, hakikuwa na kitanda.

"Mwasi kamwite baba yako." Bi. Mtupeni alimwagiza binti yake "Kwani yuko wapi mzee?"

"Alitoka hapa anasema anakwenda kunywa kahawa pale barabarani na wazee wenzie."

********************************

Ilikuwa vilio. Eddy sasa alianza kazi ya kuwabembeleza. Bi. Mtupeni ndiye aliyeanza. Binti yake Mwasi alifuatia. Baadaye Mzee Digalu, akaanza kufuta machozi. Ilikuwa kama alipeleka habari ya msiba.

Haikuwa hivyo. Alichowaambia ni kwamba amemaliza kukusanya ushahidi kesi ya Tina, hivyo anatarajia kukata rufani ili isikilizwe tena kwenye Mahakama ya Rufani.

Vilikuwa vilio vya furaha na huzuni pia.

"Una uhakika atashinda kweli baba?"

"Hapana. Siyo kama atashinda. Ila tunataka haki itendeke. Tunataka wale walioshirikiana naye nao kama ushahidi utawatia hatiani, basi na wao waungane naye. Hicho ndicho kilichonivuta mimi kuiingilia kesi hii.

Na kilichonisukuma mimi ni kilio cha yule msichana Tina pale mahakamani siku ile. Kilio cha huyu wewe mama na binti yako. Iliniuma sana. Pia nilianza kuwa na shaka kama msichana kama yule anaweza kutekeleza mauaji yale bila msaada wowote wa watu wenye akili ya mambo yale." Aliwaambia.

**ITAENDELEA JUMAPILI**



# KICHAMBO CHA ZARI BALAA

Ukisikia kichambo ndio hiki! Basi bwana mzazi mwenza wa Diamond Platnumz, anayejulikana kama Zari The Boss Lady, amechafua hali ya hewa baada ya kumbwatukia mtu aliyemwambia kuwa umbo lake la sasa kamuiga Hamisa Mobetto.

Katika mwonekano wake mpya, Zari ameonekana kuongezeka eneo la mapaja na kufanya kuwa na umbo lililokatika vyema tofauti na mwanzo.

"Watu kutwa wananiongelea mimi, unajua punguza mawazo, huna nuru hebu niangalie mimi ninavyowaka. Unaumia na maisha ya watu, huna la kutuambia maneno tumeyaachia hapo," amesema kupitia akaunti yake ya Instagram.




# VIDEO YA MWAMBIENI SHIDA TUPU

KWELI mwenye nacho huongezewa! Usemi huo unadhihirishwa na mwanamuziki kutoka lebo ya WCB, Zuchu, ambaye licha ya kuongoza kwa kufanya vizuri sasa amewapiga nyingine na kuibua tafrani.

Video ya wimbo wake mpya 'Mwambieni' ambayo tangu iachiliwe ina siku kama tano hivi, imewasha moto katika mtandao wa You tube, kiasi cha muda huo mchache pekee amefanikiwa kupata watazamaji wanaokaribia milioni moja.

Baadhi ya mashabiki wa muziki wamesema video hiyo imetengenezwa katika hali ya kawaida, lakini imeweza kuwashika watu vilivyo.

# Ferooz akumbuka mpenzi wake alipomkimbia

MKONGWE wa muziki wa Bongo Fleva, Ferooz, amesema wimbo wake 'Bilionea' unaakisi maisha yake halisi kiasi wakati mwingine akiimba anatokwa na machozi.

Amesema katika maisha yake baada ya kushuka kiuchumi amepitia mengi, ikiwamo kukimbiwa na mpenzi wake pamoja na marafiki zake wa karibu.

"Tulikuwa tumepanga mambo mengi ya maisha, lakini alipoona pesa sina aliondoka na kuniacha peke yangu, naamini wimbo wangu huu utarudisha maisha yangu ya nyuma na kunipatia furaha," amesema Ferooz.



# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### ARAUJO ATAKIWA MAN CITY
KLABU ya Manchester City ina nia ya kumsajili beki wa kati wa Uruguay, Ronald Araujo mwenye umri wa miaka 22, ambaye amesitisha mazungumzo ya kuongeza mkataba na Barcelona. ***(Sport)***

### ARAUJO AWANIWA
MANCHESTER United pia wanajiandaa kutuma ofa ya kumnunua, Ronald Araujo mwenye umri wa miaka 22, ambaye mkataba wake wa Barcelona unamalizika mwaka 2023. ***(Marca)***

### DE LIGT ACHEZA 36
MLINZI wa Juventus, Matthijs De Ligt alishiriki mechi 36 za klabu hiyo baada ya kukosekena mwanzoni mwa msimu kwa sababu ya jeraha la bega. ***(Sport)***

### TIMU ZAMGOMBEA
MANCHESTER United iko tayari kuchuana na Bayern Munich na Barcelona katika kinyanganyiro cha kumsajili Matthijs de Ligt mwenye umri wa miaka 22 kutoka Juventus. ***(Calciomercato)***

### MAN YASAKA WALINZI
MANCHESTER United wanapanga kurekebisha safu yao ya ulinzi kwa kumsajili Declan Rice wa West Ham mwenye umri wa miaka 23 na Kelvin Phillips mwenye umri wa miaka 26 kutoka Leeds United. ***(ESPN)***

### RUDIGER MAMBO BADO
KLABU ya Chelsea ilishindwa katika jaribio lake la kumuongezea mkataba mpya mlinzi wa Ujerumani, Antonio Rudiger mwenye umri wa miaka 28, huku Real Madrid na Paris St-Germain zikiwa na nia ya kutaka kumsajili. ***(Mail)***

### DELE ALITAKIWA UTURUKI
RAIS wa timu ya Adana Demirspor, Murat Sancak anadai klabu hiyo ilikubali kumsajili Dele Alli kwa mkopo kutoka Tottenham Hotspur kabla ya raia huyo wa England mwenye umri wa miaka 25 kujiunga na Everton kwa mkataba wa miaka miwili na nusu. ***(Milliyet)***

### SAKA KUONDOKA ARSENAL
KLABU za Liverpool na Manchester City zinaweza kumnunua winga wa England, Bukayo Saka mwenye umri wa miaka 20, ikiwa Arsenal itashindwa kufuzu Ligi ya mabingwa Ulaya msimu ujao. ***(ESPN)***

### WATFORD ILISHINDWA
KLABU ya Watford ilishindwa na mbinu ya kumsajili beki wa Manchester United, Phil Jones mwenye umri wa miaka 29, kabla ya dirisha la usajili la Januari kufungwa. ***(Football Insider)***

### CADAMARTERI AGOMBEWA
MANCHESTER City wameungana na West Ham na Brentford kuonesha nia ya kumnunua mshambuliaji wa kimataifa wa England mwenye umri wa miaka 16, Bailey Cadamarteri. ***(Sheffield Star)***

### CASH AWANIWA ATLETICO
KLABU ya Atletico Madrid bado "wanatamani sana" kumsajili beki wa Aston Villa kutoka Poland, Matty Cash mwenye umri wa miakaa 24, kabla ya msimu ujao. ***(Fabrizio Romano)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MANE: TUNATAKA UBINGWA AFCON KWA AKILI YA KOCHA

●●●Wachezaji wajipanga kulibeba taji hilo wakati wakiikabili Misri kwenye fainali ya kibabe...

**YAOUNDE, Cameroon**

SADIO Mane na Edouard Mendy wamesema Senegal inataka kupunguza presha kwa Kocha, Aliou Cisse kwa kushinda taji la mataifa ya Afrika, Afcon, leo Jumapili wakati wakicheza fainali na Misri.

Senegal, ambao ni washindi wa pili wa michuano hiyo mwaka 2019, walikuwa miongoni kwa timu zilizokuwa zinapewa nafasi kubwa kabla ya kuanza kwa mashindano hayo, lakini walianza kwa kusuasua.

Simba hao wa milima ya Teranga walianza kwa ushindi mwembamba dhidi ya Zimbabwe na baadae wakafuatiwa na suluhu dhidi ya Guinea na Malawi kwenye kundi B, ambapo Kocha Cisse alianza kushutumiwa.

Lakini uwezo binafsi wa fowadi wa Liverpool, Mane uliisaidia Senegal kupata ushindi dhidi ya Cape Verde, Equatorial Guinea na Burkina Faso na kutinga fainali.

"Naamini mtu huyu (Aliou Cisse) anastahili kila kitu kwa sababu ndie kocha anayeshutumiwa sana, lakini hakati tamaa," alisema Mane akiiambia BBC Sport Africa.

"Anajiamini yeye mwenyewe, analiamini kundi hili. Amekuwa akishutumiwa nje ya uwanja, lakini hapa anafanya kazi kubwa.

"Kitu muhimu zaidi tunataka kushinda taji kwa ajili yake na nchi yetu kwa sababu anastahili hicho baada ya kupitia kila kitu kuanzia akiwa mchezaji wa Senegal na sasa kocha.

"Litakuwa jambo kubwa kumzawadia taji la mashindano haya kwake na nchi yetu."

Cisse alicheza mechi 35 kwa Senegal wakati wa uchezaji wake na alikuwa nahodha wa timu hiyo kwenye michuano ya kombe la Dunia mwaka 2002 wakati walipowafunga waliokuwa mabingwa watetezi Ufaransa kwenye mchezo wa kwanza na waliishia robo fainali.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI

SENEGEAL
VERSUS
EGYPT

1 | 2.06
X | 2.87
2 | 4.25

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



## POCHETTINO AKARIBIA KUTUA MAN UNITED

**PARIS, Ufaransa**

KLABU ya Paris Saint-Germain na Mauricio Pochettino wanakaribia kufikia makubaliano ya maelewano kuangalia namna kocha huyo raia wa Argentina anaondoka pale Parc des Princes mwishoni mwa msimu huu, kwa mujibu wa 90min.

Pochettino aliwasili PSG Januari 2021, na awali uteuzi wake ulionekana kuwa mzuri, lakini kushindwa kwake kutwaa taji la Ligi Kuu ya Ufaransa, Ligue 1, kwenye msimamo wake kulisababisha sintofahamu.

Wakati timu hiyo ikiwa inaongoza msimamo kwa tofauti ya pointi 11 baada ya mechi 22 msimu huu, majaliwa ya Pochettino kuendelea kuwepo hapo Paris yanaonekana kuwa na kizungumkuti.

Timu yake imekuwa na wakati mgumu ndani ya dimba na inaonekana kama vile anashindwa kukipanga kikosi vizuri ambacho kimesheheni nyota kibao na walitolewa na Nice kwenye kombe la Ufaransa.

Usajili wa Lionel Messi kutoka Barcelona kipindi cha majira ya joto kilichopita nalo linaonekana kuwa tatizo jingine.

Na sasa kwa mujibu wa ripoti hiyo, Pochettino mwenye umri wa miaka 49 ana nafasi kubwa ya kwenda kuwa kocha mkuu wa Man United baada ya kutimuliwa kwa Ole Gunnar Solskjaer, Novemba mwaka jana.

Man United baada ya kumfukuza Solskjaer walimchukua Ralf Rangnick ambaye anainoa timu hiyo kwa muda hadi mwisho wa msimu huu.

## Klabu tano zamgombea Haaland



**DORTMUND, Ujerumani**

KLABU tano za Ulaya zipo kwenye harakati za kuwania kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Erling Haaland

Gazeti la Marca la Hispania limeripoti kuwa Real Madrid na Barcelona zinachuana vikali kumnasa mchezaji huyo, lakini pia klabu za Ligi Kuu England, Manchester City na Chelsea vina nia ya kumsajili.

Uwezekano mwingine kwa Haaland kusajiliwa ni Paris Saint-Germain ambayo italazimika kusajili mbadala wa Kylian Mbappe iwapo ataondoka mwishoni mwa msimu huu.

Man City ina uhitaji mkubwa wa kusajili mshambuliaji baada ya Sergio Aguero na Ferran Torres kuondoka na pia walishindwa kumsajili Harry Kane msimu uliopita.

Wakala wa Haaland, Mino Raiola atafurahi kuona nia hizo zinafanikiwa huku klabu za Ulaya zikilazimika kulipa ada na bonasi nono ili kupata saini yake.

HABARI MICHEZO

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# MASHINDANO YA GOLFU KUKUSANYA SH. MIL. 40

**Na Mary Geofrey**

KLABU ya Rotary Tawi la Bahari, imefanya mashindano ya mchezo wa Golfu kwa ajili ya kukusanya Sh. milioni 40 zitakazosaidia kuboresha mazingira ya kusomea na kufundishia wanafunzi katika Shule ya Sekondari Mtakuja.

Mashindano hayo yalifanyika jana jijini Dar es Salaam, katika viwanja vya Gymkhana na kuhudhuriwa na wanamichezo mbalimbali.

Rais wa Klabu ya Rotary, Tawi la Bahari, Rotarian Diamond Carvalho, akizungumza na waandishi wa habari wakati mashindano hayo yakiendelea, alisema fedha watakazokusanya zitanufaisha watoto 1,500 wanaoishi katika Kampasi yao.

Alisema jumuiya ya Rotary kwa kushirikiana na jumuiya ya wafanyabiashi wameshirikiana kukusanya fedha hizo ambazo zitasaidia kuboresha mifumo ya maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya shule hiyo ili kuwakinga na magonjwa yanayotokana na kukosekana kwa maji safi.

Alisema wanafunzi hao wakipata huduma za majisafi na salama wataweza kuhudhuria vyema masomo yao na kufaulu masomo yao.

Carvalho alisema pia mradi huo una lenga kukarabati madarasa na kununua madawati na kusaidia huduma ya uchapaji wa mahitaji ya wanafunzi.

Alisema miaka 10 iliyopita walifanya mashindano ya Golfu yaliyosaidia kukusanya Sh milioni 300 zilizosaidia katika miradi mbalimbali inayotekelezwa na klabu hiyo.

Alisema mradi uliopita walikuwa wakisaidia elimu, michezo, ubunifu na ujenzi wa maktaba za shule na kununua vitabu vya kuweka katika maktaba na kuwawezesha vijana kiuchumi.

Naye Kepteni wa mchezo wa Golfu wa Gymkhan, Fredy Laiza, alisema wamefanya mashindano kwa ajili ya kukusanya kiasi hicho cha fedha za kusaidia shughuli za jamii.

Alisema mashindano hayo yalipaswa kufanyika mwaka jana lakini ilishindikana kwa sababu ambazo zilikuwa nje ya uwezo wao na kwamba yalienda vizuri huku washiriki wakifurahia hali ya hewa iliyokuwapo.



Mchezaji wa timu ya KMC ya Vijana (katikati), akimiliki mpira huku akizongwa na wachezaji wa timu ya Azam ya vijana katika mchezo wa kirafiki uliopigwa Uwanja wa Chamazi jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mo Dewji akunwa na Simba Queens

**Na Saada Akida**

RAIS wa heshima wa Simba, Mohammed Dewji amewapongeza wachezaji wa Simba Queens na kudai anajivunia na matokeo wanayoyapata katika michezo yao ya Ligi Kuu ya wanawake Tanzania.

Kauli hiyo ni baada ya timu hiyo ya wanawake kuendelea kupata matokeo mazuri baada ya juzi kuibuka na ushindi wa mabao 7-0 dhidi ya JKT Queens, mchezo uliopigwa uwanja wa Mo Arena.

Wakati Dewji akitoa pongezi na kujivunia kwa mwenendo wa Simba Queens, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Sebastian Nkoma amesema ana matarajio na wachezaji wake kufanya vizuri na kuendelea kuwapa raha wanasimba.

Alisema kazi kubwa ni kuhakikisha anafanyia kazi mapungufu ya timu yake na kujiimarisha na kuendelea kupata matokeo mazuri katika michezo yao ijayo.

"Natambua ligi ina ushindani mkubwa sasa tumefanikiwa kushinda mechi zote tisa na kuhakikisha tunafanya maandalizi mazuri na kuendelea kuwapa furaha na raha wanasimba hasa wakati huu wanaoupitia sasa kwa timu kubwa," alisema Nkoma.

Alisema wanapambana kutafuta matokeo mazuri katika michezo yao kwa ajili ya kupata pointi muhimu katika kila mechi na kuwataka mashabiki wa Simba kuwaunga mkono Simba Queens.

Simba Queens ni mabingwa watetezi na inaongoza msimamo kwa kujikusanyia pointi 27 katika michezo 9 ya Ligi Kuu ya wanawake Tanzania Bara.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## JUMAPILI - 06/02/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:15 | 1648 | Feyenoord vs Sparta Rotterdam | 1.23 | 5.68 | 10.77 |
| 14:30 | 4653 | Atalanta vs Cagliari | 1.25 | 6.21 | 10.01 |
| 15:00 | 4586 | Lorient vs Lens | 3.19 | 3.44 | 2.17 |
| 15:00 | 5680 | Liverpool vs Cardiff | 1.11 | 7.91 | 21.76 |
| 15:30 | 5978 | Brugge vs KAA Gent | 2.26 | 3.51 | 2.87 |
| 16:00 | 1679 | AEK Athens vs Apollon Smyrnis | 1.26 | 5.31 | 10.82 |
| 16:00 | 1733 | Valencia vs Real Sociedad | 2.79 | 3.24 | 2.54 |
| 16:00 | 5188 | Orlando Pirates vs Amazulu | 1.99 | 2.90 | 3.96 |
| 16:00 | 5223 | Caykur Rizespor vs Adana Demirspor | 3.01 | 3.31 | 2.27 |
| 16:15 | 5130 | FC Basel vs FC Sion | 1.48 | 4.55 | 5.54 |
| 16:30 | 3536 | Motherwell vs Celtic | 8.31 | 4.85 | 1.34 |
| 17:00 | 1335 | Zlin vs Slovan Liberec | 2.27 | 3.30 | 3.15 |
| 17:00 | 1771 | Bologna vs Empoli | 2.01 | 3.74 | 3.39 |
| 17:00 | 1937 | Sampdoria vs Sassuolo | 2.80 | 3.64 | 2.34 |
| 17:00 | 2337 | Reims vs Bordeaux | 2.11 | 3.38 | 3.38 |
| 17:00 | 2696 | Troyes vs Metz | 2.04 | 3.43 | 3.53 |
| 17:00 | 3588 | Strasbourg vs Nantes | 1.78 | 3.63 | 4.38 |
| 17:00 | 4560 | Nice vs Clermont Foot | 1.58 | 4.07 | 5.36 |
| 17:00 | 5829 | Venezia vs Napoli | 6.79 | 4.70 | 1.43 |
| 17:30 | 3035 | Borussia Dortmund vs Bayer Leverkusen | 1.92 | 4.08 | 3.34 |
| 18:00 | 3029 | Mechelen vs Kfco Wilrijk | 1.87 | 3.80 | 3.60 |
| 18:15 | 4029 | Barcelona vs Atletico Madrid | 2.39 | 3.27 | 2.98 |
| 18:15 | 4609 | Ionikos Nikea FC vs Olympiakos | 8.91 | 4.55 | 1.35 |
| 18:30 | 1392 | RB Salzburg vs LASK Linz | 1.24 | 5.60 | 8.49 |
| 18:30 | 1761 | Gil Vicente vs Santa Clara | 2.11 | 3.21 | 3.45 |
| 18:30 | 1773 | Boavista vs FC Vizela | 2.17 | 3.21 | 3.31 |
| 18:30 | 4741 | FC Lugano vs FC Luzern | 2.00 | 3.45 | 3.50 |
| 18:30 | 5200 | St. Gallen vs BSC Young Boys | 4.64 | 4.14 | 1.62 |
| 18:45 | 4819 | Ajax vs Heracles Almelo | 1.06 | 10.75 | 25.41 |
| 19:00 | 1261 | Rangers vs Hearts | 1.40 | 4.52 | 7.27 |
| 19:00 | 1529 | Nottingham vs Leicester | 3.35 | 3.45 | 2.05 |
| 19:00 | 1547 | Goeztepe vs Altay | 1.90 | 3.55 | 3.74 |
| 19:00 | 3894 | Besiktas vs Antalyaspor | 1.78 | 3.61 | 4.25 |
| 19:00 | 5072 | Rennes vs Brest | 1.49 | 4.38 | 5.98 |
| 19:05 | 4883 | Istra vs Dinamo Zagreb | 9.46 | 5.41 | 1.24 |
| 19:30 | 2328 | VfL Wolfsburg vs Greuther Furth | 1.57 | 3.99 | 5.58 |
| 20:00 | 2204 | Viktoria Plzen vs Hradec Kralove | 1.39 | 4.81 | 7.42 |
| 20:00 | 2495 | Udinese vs Torino | 3.00 | 3.20 | 2.41 |
| 20:30 | 3865 | PAOK vs Panathinaikos | 1.90 | 3.30 | 4.04 |
| 20:30 | 3902 | Anderlecht vs Eupen | 1.32 | 5.10 | 8.05 |
| 20:30 | 4701 | Betis vs Villarreal | 2.37 | 3.50 | 2.85 |
| 20:30 | 5869 | Lamia vs Asteras Tripolis | 3.05 | 3.00 | 2.41 |
| 21:00 | 1552 | FC Arouca vs Porto | 8.92 | 5.35 | 1.29 |
| 21:30 | 4473 | Bournemouth vs Boreham Wood | 1.26 | 5.34 | 10.88 |
| 22:00 | 3437 | Senegal vs Egypt | 2.06 | 2.87 | 4.25 |
| 22:45 | 2004 | Lille vs Paris St Germain | 3.73 | 3.59 | 1.93 |
| 22:45 | 3568 | Juventus vs Verona | 1.61 | 3.99 | 5.32 |
| 23:00 | 2745 | Racing Genk vs Zulte Waregem | 1.32 | 5.32 | 7.69 |
| 23:00 | 4104 | Real Madrid vs Granada | 1.29 | 5.65 | 9.10 |
| 23:30 | 5825 | Sporting Lisbon vs Famalicao | 1.34 | 4.82 | 8.27 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Jumapili Februari 6, 2022

Nipashe




## Mane: Tunataka ubingwa Afcon kwa akili ya kocha

HABARI UK 21



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Senegal wakifanya mazoezi ya mwisho kujiandaa na mchezo wa fainali ya mataifa ya Afrika, Afcon, dhidi ya Misri utakaopigwa leo nchini Cameroon. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA YAIWINDA MBEYA KWANZA

Ni katika mchezo wa leo unaotazamiwa kuwa na upinzani mkali, Wekundu wa Msimbazi wakipanga kuondoka na pointi zote tatu, huku...

**Saada Akida na Adam Fungamwango**

SIMBA inakibarua kigumu kingine leo kutafuta pointi tatu muhimu dhidi ya Mbeya Kwanza, mchezo wa Ligi Kuu Tanzania utakaochezwa saa 1:00 usiku, Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Huo ni mchezo muhimu kwa kila timu huku Simba ikiendelea kutafuta matokeo chanya ili kupata pointi tatu kwa ajili ya kupunguza wigo mpana na pointi 10 walizopitwa na wapinzani wao Yanga inayoongoza ligi hiyo.

Simba ikipambana kutafuta pointi tatu ili kutetea ubingwa wao ,Mbeya Kwanza wanachanga karata zao vizuri ili kujinasua kwenye mtego wa nafasi ya 12 na kupanda juu katika msimamo.

Akizungumzia mchezo huo, Kocha msaidizi wa Simba, Selemani Matola alisema wamefanya maandalizi ya kutosha na wapo tayari kuivaa Mbeya Kwanza.

Alisema hautakuwa mchezo rahisi kwa sababu Mbeya Kwanza wako vizuri na wanaenda kupambana kuhakikisha wanatumia vema nafasi wanazopata na kufunga mabao mengi.

"Tumejiandaa vizuri na kurejea kwa Sadio Kanoute na Jonas Mkude kumeimarisha kikosi chetu na kuhakikisha tunaenda kutafufa pointi tatu muhimu katika mbio zetu za ubingwa," alisema Matola.

Kwa upande wa Kocha msaidizi wa Mbeya Kwanza, Nizar Khalifan alisema wamejiandaa vizuri kucheza na Simba na wanaimani utakuwa mchezo wa ushindani mkubwa kwao.

"Tumejiandaa vizuri na tunajiandaa kutafuta matokeo chanya, mechi itakuwa ya ushindani mkubwa kwa sababu kila mmoja wetu anahitaji kupata pointi muhimu katika mchezo huu," alisema Nizar.

Nahodha wa Mbeya Kwanza, Salum Chuku alisema wanawaheshimu Simba na wamejipanga vizuri na wana imani wanaenda kupambana kutafuta matokeo mazuri.

"Kama wachezaji tumezungumza na kuhakikisha tunaleta upinzani mkubwa mbele ya Simba ili kuondoka na pointi muhimu katika mchezo huu," alisema Chuku.

Wakati Simba ikishinda mechi moja, kwenye mechi nne zilizopita, ikitoka sare mbili, Mbeya Kwanza imetoka sare mbili, kufungwa moja na kushinda moja kwenye mechi zake nne zilizopita.

Hata hivyo, mara ya mwisho Simba kushinda ilikuwa Alhamisi iliyopita, Mbeya Kwanza ilikuwa ni Desemba 22 mwaka jana, ilipowafunga wababe wa Wekundu hao wa Msimbazi, Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba mkoani Kagera, mabao 2-0.

Ilitoka sare ya bao 1-1, dhidi ya KMC, 1-1 dhidi ya Geita Gold na kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC.

## Nabi: Yanga mambo bado

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi amesema licha ya kuongoza msimamo kwa pointi 35 bado ubingwa ni kitendawili na amewataka wachezaji kuwa makini na kujituma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema ligi sio nyepesi kwa kuwa kila timu imejipanga kupata pointi tatu na kwa sababu ya ugumu huo wanatakiwa kupambana katika kila mechi.

Alisema kutopoteza mechi na kuongoza ligi kwa pointi 10 sio kwamba wamemaliza kazi, na kuona bado ana kazi kubwa kwa wachezaji wake kuhakikisha wanapambana kutafuta matokeo kila mechi.

"Ligi ni ngumu na hakuna mchezo mwepesi ambao tunakutana nao hilo lipo wazi kuwa kila timu tunayocheza nayo inahitaji ushindi na hakuna timu ambayo ni rahisi," alisema Nabi.

"Kikubwa ni kuona tunapata matokeo chanya nasi ili kupata pointi hakuna namna nyingine unayotakiwa kufanya zaidi ya kutafuta ushindi," aliongeza.

Alisema wachezaji wanatakiwa kuwa makini na kuzingatia maelekezo na kila mmoja anatakiwa kupambana mazoezini ili kupata nafasi ya kucheza.

"Ligi ni ngumu sana, hakuna mechi iliyokuwa rahisi mbele yetu, tunatakiwa kuwaheshimu wapinzani wetu, kwa sababu kila timu imejipanga kutafuta pointi tatu kwa kila mechi."

Alisema anasisitiza sana wachezaji wake kuzingatia anayowapa mazoezini kuyafanyia kazi katika mechi lakini pamoja na kucheza kitimu ili kufikia malengo yao.

**"Hatuwezi kujisifia kwamba tunachukuwa ubingwa mbali ya kuwa tunaongoza , ligi ni ngumu na ushindani ni mkubwa, wachezaji wanatakiwa kujituma na kucheza kwa ushirikiano mkubwa ili kufikia malengo ya kutwaa ubingwa wa Ligi hiyo."**

9 770856 541002 >

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, SL P 9